



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

VOL. LXII, No. 22

GAZETI

29 MEI, 1981

BEI SH. 3/-

Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na
Limeandikishwa Posta kama
Gazeti

DAR ES SALAAM

YALIYOMO

Taarifa ya Kawaida Uk.

Kuajiriwa na Kukabidhiwa Ma	...	Na. 513	237
Notice re Supplement	...	Na. 514	238
Tanzania	...		238
Siku ya Uteuzi wa Mwanzo—Uchaguzi wa Bunge—Mtwara Vijijini	...	Na. 515	238
Kupotea kwa Hati ya Bima	...	Na. 516-7	238
Ofisi ya Mrajis Msa'dizi wa Vyama vya Ushirika—Songea, Ruvuma	...	Na. 518	238
Muunganisho wa Wadhamini	...	Na. 519	238
Maombi ya Bonasi—Kiwanda cha Kioo	...	Na. 520	239
Maombi ya Kuandikisha Lengo—General Food na JUWATA	...	Na. 521	239

Taarifa ya Kawaida Uk.

Mahakama ya Kazi—Mkataba wa Hiari baina ya JUWATA na Tanzania Food Corporation	...	Na. 522	240/3
Mgogoro wa Kazi—Zambia Tanzania Road Service Dar es Salaam	...	Na. 523	244/9
Hati za Uvumbuzi	...	Na. 524	249
Kampuni Zinazotarajiwa Kufutwa katika Daftari la Makampuni	...	Na. 525	249
Alama za Biashara	...	Na. 526	249
Alama za Biashara Zilizoandikishwa katika Daftari	...	Na. 527	250
Maombi ya Leseni za Magari ya ab'ria, Uchukuzi wa Mizigo na Mabadiliko ya Leseni	...	Na. 528-9	250/1
Uthibitisho na Usimamiaji wa Mirathi	...	Na. 530-1	251/2

KUAJIRIWA NA KUKABIDHIWA MADARAKA

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 513

Ofisi ya Makamu wa Rais: (Wizara ya Mipango na Uchumi):

Kuwa Wachumi, Daraja la III:—

E. W. TONDI, Mwalimu, Daraja la (d), kuanzia tarehe 14 Machi, 1980.

G. N. NAMWAMBE, kuanzia tarehe 30 Aprili, 1980.

Bi. D. MLINGA, kuanzia tarehe 3 Mei, 1980.

Bibi J. H. LEMA, kuanzia tarehe 1 Septemba, 1980.

D. NYAMAGANDA, kuanzia tarehe 18 Oktoba, 1980.

A. B. S. MATEMU, kuanzia tarehe 5 Novemba, 1980.

R. M. KHIJAH, Mtakwimu, Daraja la II, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1981.

Kuwa Mtakwimu, Daraja la I:—

P. N. NDIMILA, Afisa Takwimu, Daraja la I, kuanzia tarehe 1 Januari, 1981.

Ofisi ya Waziri Mkuu:

Kuwa Muuguzi/Mkunga:—

ANGELINA SHIJA, kuanzia tarehe 3 Februari, 1981.

Kuwa Muuguzi:—

JACOB I. MASABA, kuanzia tarehe 27 Machi, 1981.

Kuwa Waganga Wasaidizi Vijijini (Rural Medical Aids):—

M. KANYASA, kuanzia tarehe 1 Machi, 1981.

J. Y. MALAGI, kuanzia tarehe 1 Machi, 1981.

M. N. MUZAZI, kuanzia tarehe 1 Machi, 1981.

Kuwa Technicians (Buildings), Grade III:—

W. KASWAGA, Technician (Buildings), Grade IV, kuanzia tarehe 1 Januari, 1981.

A. A. SIANGA, Technician (Buildings), Grade IV, kuanzia tarehe 1 Januari, 1981.

N. G. KAMGUNA, Technician (Buildings), Grade IV, kuanzia tarehe 1 Januari, 1981.

M. S. NDAMBACHIA, Technician (Buildings), Grade IV, kuanzia tarehe 1 Januari, 1981.

Kuwa Meneja wa Kijiji, Daraja la V:—

EDNA GABONE, Registry Assistant, kuanzia tarehe 11 Januari, 1981.

Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka—(inaendelea tazama ukurasa wa 252)

Matangazo yahasuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma, yaweza kuchapishwa katika *Gazeti*. Matangazo yote yapelekwe kwa Mhariri, Idara ya Habari (Schemu ya Uchapishaji) S.L.P. 9142, Dar es Salaam, Simu za Ofisi 31817 na 25375. kabla ya Jumanne ya kila Juma. Matangazo yasipelekwe kwenye Wizara ya Maendeleo ya Utumishi wala Idara ya Kupiga Chapa.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 514

Notice is hereby given that, Rules, Rules of Court and a Notice, as set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 22, to this number of the *Gazette*.—

Rules under the Judicature and Application of Laws Ordinance (Government Notice No. 64 of 1981).

Rules under the Appellate Jurisdiction Act, 1979 (Government Notice No. 65 of 1981).

Rules of Court under the Elections Act, 1970 (Government Notice No. 66 of 1981).

Notice under the Standards Act, 1975 (Government Notice No. 67 of 1981).

TANZANIA

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea kwenye Kambi ya Polisi, Kigoma tarehe 21 Aprili, 1981 cha Ndugu ALINANINE AMBENGE, askari wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea kwenye Hospitali ya Bugando, Mwanza tarehe 16 Aprili, cha Ndugu HENRY MSEKWA, askari wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea kwenye Hospitali ya Kiteto, Tabora tarehe 10 Aprili, 1981 cha Ndugu ALPHONCE HITLER MARISHALI, Koplo wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea huko Musoma tarehe 25 Machi, 1981 kwa ugonjwa cha Ndugu YOHANA NGUTU, Koplo wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha aliyekuwa Afisa Maslahi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndugu BUNDARA YUSUFU HAMISI, Assistant Fisheries Officer, Grade I, kilichotokea tarehe 8 Mei, 1981 kwa ajali ya pikipiki katika njia panda ya barabara ya Chang'ombe na Mowlem, kwenye taa za barabarani karibu na Kituo cha Polisi Chang'ombe.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 515

SIKU YA UTEUZI WA MWANZO

UCHAGUZI WA BUNGE WILAYA YA MTWARA VIJILINI

Sheria ya Uchaguzi

(Na. 25 ya 1970)

(Fungu la 49)

Inatangazwa kwa ufahamisho wa watu wote kwamba Jumatatu, tarehe 8 Juni, 1981 inateuliwa kuwa ndio siku ya Uteuzi wa Mwanzo kwa Wilaya ya Uchaguzi ya Mtwara Vijijini, na inahitajika kwamba watu wote wanaotaka kugombea uchaguzi wawasilishe fomu zao za uteuzi wa mwanzo kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa Wilaya hiyo siku hiyo ya uteuzi wa mwanzo, kabla ya saa kumi za mchana.

Dar es Salaam,
15 Mei, 1981

Chief A. S. MKWAWA,
Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 516

KUPOTEA KWA HATI YA BIMA

NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF (T) LIMITED

(SHIRIKA LA BIMA LA TAIFA)

HATI NA. 171378 JUU YA MAISHA YA BWANA FIRMIN G. BAMBO

Taarifa imetolewa kuhusu kupotea kwa hati ya bima iliyotajwa hapo juu nakala yake itatolewa kama malalamiko kupinga kutolewa kwa hati hiyo hayakuwakilishwa kwenye Shirika hili mwezi mmoja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

S.L.P. 9264,

Dar es Salaam,
15 Mei, 1981

k.n.y. Meneja Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 517

KUPOTEA KWA HATI YA BIMA

NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF (T) LIMITED

(SHIRIKA LA BIMA LA TAIFA)

HATI NA. L/50782 JUU YA MAISHA YA BWANA MODESMO RUSHEMA

Taarifa imetolewa kuhusu kupotea kwa hati ya bima iliyotajwa hapo juu nakala yake itatolewa kama malalamiko kupinga kutolewa kwa hati hiyo hayakuwakilishwa kwenye Shirika hili mwezi mmoja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

S.L.P. 9264,

Dar es Salaam,
18 Mei, 1981

k.n.y. Meneja Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 518

OFISI YA MRAJIS MSAIDZI WA VYAMA VYA USHIRIKA, SONGEA RUVUMA

(Ibara ya 81)

Sheria ya Vyama vya Ushirika, 1968

Kifungu cha 78 (21)

(Sheria za Tanganyika)

KUMTEUA MFILISI

Kwa mujibu wa ibara ya 81 ya Sheria za Vyama vya Ushirika, 1968; Mimi L. M. RIMISHO, Msaidizi wa Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa RUVUMA namteua Ndugu M. N. NJOHOLE, Afisa Ujamaa na Ushirika (W) Songea Vijijini, kuwa Mfilisi wa Vyama vya Msingi vilivyofutwa katika Wilaya ya Songea Vijijini. Uteuzi wa Ndugu EMIL ANDREW MTALEMWA chini ya Taarifa ya Kawaida Na. 1373 ya tarehe 15 Oktoba, 1976 kwa minajili hii umefutwa.

Tangazo hili imetolewa nami, hapa Songea tarehe tano mwezi wa tano, mwaka elfu moja mia tisa themani na moja.

L. M. RIMISHO,
Songea/Ruvuma,
5 Mei, 1981.

Msaidizi Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Ruvuma

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 519

MUUNGANISHO WA WADHAMINI

Sheria ya Muunganisho wa Wadamini

(Sura ya 375)

Taarifa inatolewa kuhusu mabadiliko ya jina la Muunganisho kama ifuatavyo:—

Kutoka Jina la:

Kuwa Jina la:

THE REGISTERED TRUSTEES OF THE BOHORA GYMKHANA TANGA.

THE REGISTERED TRUSTEES OF SHABAB GYMKHANA TANGA.

Dar es Salaam,
21 Aprili, 1981

K. P. KOBELO,
Msimamizi Mkuu wa Wadamini

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 520

MAOMBI YA BONASI

(Na. 4 ya 1980-

Sheria ya Mahakama ya Kazi

(Na. 41 ya 1967)

*Wanaohusika: KIWANDA CHA KIOO LIMITED**Mahakama ya Kazi:*

Mbele ya:—

J. J. MACKANJA, Naibu Mwenyekiti.
Ndugu MTUMBUKA, Mshauri—A.T.E.
Ndugu MANYONYI, Mshauri—JUWATA.

Kuwakilisha JUWATA:

OMARI SEIF, Mwenyekiti Kiwandani.
SAID ATHUMANI, Katibu Kiwandani.

Kuwakilisha Waajiri:

Ndugu AKIDA, Meneja Utumishi.

TUZO

Katika lengo lao lililosajiliwa na Mahakama Messrs. Kioo Ltd. walitarajia kuzalisha glass tani 9,500 ambacho ni zaidi ya kama tani 1,000 hivi katika uzalishaji wao mwaka 1977. Lakini kutokana na bidii yao waliweza kuzalisha tani 10,493, ambalo ni onge eko la tani kama 1,000 hivi. Hili ni ongezeko la kuridhisha ingawa tuta-kavyoona baadaye, thamani yake ni ndogo kulinganisha na mauzo yaliyokadirwa.

Jambo jingine la kuwapongeza menejimenti pamoja na wafanyakazi ni kuweza kwao kudhiti gharama za uzalishaji. Ingawa walikadira gharama hizo kufikia Sh. 31,504,596/- walikaa Sh. 28,446,718/- tu. Hata hivyo kiasi hiki ni kama 25.9% ya mauzo ya 1977.

Nimesema kwamba mauzo yao yalishuka. Waombaji walikadira kupata Sh. 34,020,328/- lakini kiasi halisi walichopata ni Sh. 28,930,233/- tu. Sababu l'yoathiri mauzo ni juhudi yao ya kutengeza chupa za bia zaidi ambazo thamani yake ni ndogo bada'a ya kusisitiza uzalishaji wa ana nyengine ya glass ambayo ina thamani kubwa. Jitihada ya kuzalisha glass yenye rangi, walivyosema waajiri, ilikuwa kusaidia kutokwamisha uzalishaji wa Kampuni ya Bia. Mahakama inaikubali sababu hiyo kama ya kimsingi na yenye kuzingatia ufanisi wa vyombo vingine vya uzalishaji hapa nchini. Ushirikiano huo ni mzuri na yafaa udumishwe kati ya makampuni mengine yaliyo na shughuli zinazotegemeana.

Kiwanda hiki pia kimevudu kuongeza matumizi ya uwezo wa mtambo (plant capacity) kutoka 78.5% mwaka 1977 hadi 86% mwaka wa lengo.

Pamoja na hayo, tukchukua kwamba mtu-saa zilizo-tumika ni 1,734,557, tunakuta kwamba uwiano wa ufanisi wa kazi (Labour productivity ratio) ni 1:0.006 ukilinganisha na lengo la 1:0.0085. Hii inaonyesha kwamba palikuwa na uzembe kazini, jambo ambalo wafanyakazi hawapaswi kufanya. Imeonekana pia kwamba mtaji us'ondosheka (fixed assets) na mtaji wa muda mfupi (current assets) haikutumiwa vema na kwa faida ya kampuni. Tukchukua kwamba fixed assets ya Sh. 22,963,759/- ni 88.6% ya mauzo na kwamba uwiano wa faida ghafi ya Sh. 6,195,213/- na mauzo ni 1:312.8 na kwamba fixed assets ni 88.6% ya mauzo, basi kiwanda hiki lazima kijirekebesheli k'pate faida kubwa zaidi.

Kutokana na sababu mbali mbali ambazo nimetaja faida ya Kiwanda baada ya kodi ni Sh. 90,000/- ikiilinganishwa na Sh. 586,145/- mwaka 1977 au Sh. 1,257,866/- kama walivyojweka kama lengo. Kama tutachukua kukuwa kwa faida tu kama kipimo pekee cha ufanisi wa uzalishaji, basi maombi haya hayana budi kukataliwa.

Tumefikira sana juu ya suala hili na kuona kwamba uamuzi kama huo utawfisha moyo mafanyakazi ambao wamemudu kuzalisha glass tani 1,000 juu ya lengo lao. Kwa hiyo upungufu wa faida hautokani na kuzalisha mali kdogo. Katika hali hii wafanyakazi wanastahili pongezi kwa uwezo wao wa kuvuka lengo la uzalishaji walilojweka.

Kwa hiyo Mahakama inatoa tuzo kwamba kila mfanyakazi wa kudumu, ambao ni Administration—57 na Operative 188, jumla ni 245 kwa mwaka wa lengo 1978, apewe bonus ya Sh. 200/- ambacho ni kiasi cha jumla ya Sh. 29,000/-.

Imetolewa leo tarehe 20 Machi, 1981 na inakuwa na nguvu mara moja.

Dar es Salaam,
20 Machi, 1981

J. J. M. MACKANJA,
Naibu Mwenyekiti,
Mahakama ya Kazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 521

MAOMBI YA KUANDIKISHA LENGU

Na. 15/80

baina ya

GENERAL FOOD COMPANY LIMITED—DAR ES SALAAM

na

JUMUIYA YA WAFANYAKAZI TANZANIA (JUWATA)

Mahakama:

J. J. M. MACKANJA (Naibu Mwenyekiti).
G. M. MANYONYI (Mshauri)—JUWATA.
A. MWAKILIMA (Mshauri—A.T.E.).

JUWATA:

NGULLA—Mchumi.
T. WALEMA—(Mwenyekiti).

Menejimenti:

G. J. KOMBE—Meneja Mkuu.
C. WAGOFYA—Mhasibu Mkuu.
C. B. MOLOMA—Meneja Mwendeshaji.

TUZO

Uchambuzi wa takwimu za lengo hili inaonyesha kwamba mauzo ya 1979/80 ni Sh. 250,965/- na katika lengo ni Sh. 530,968m/-.

Faida ghafi imekuwa ikipanda hadi kufikia 22,555m/- na katika mwaka wa lengo inatarajiwaa kufika Sh. 54.90m/-. Faida baada ya kodi imekuwa ikipanda pia.

Mauzo kwa kila mtumishi yamekuwa yakiongezeka kwa wastani. Mwaka huu kila mfanyakazi anategemewa kuzalisha Sh. 3.179m/-.

Tija inaonyesha kwamba kila Sh. 01/- ya mshahara itazalisha Sh. 180/72.

Hata hivyo yapo matatizo kadha ambayo yataipunguza kampuni mapato na faida. Tatizo hili linahusu kuondolewa baadhi ya bidhaa (deconfinement) ambazo zilikuwa zikuzwa kupita kampuni.

Nd'yo maana ilibidi lengo lipunguwe hadi Sh. 409,506m/- kutoka Sh. 530,968m/-. Tatizo jingine ni kuondolewa mikopo ya benki (overdraft facilities) ngawa Kampuni za Mikoa (RTCs) huchukua mali kwa mikopo.

Pamoja na matatizo hayo wafanyakazi wana mori kiasi kwamba watawea kulifikia, na hata kulipita lengo lao. Kwa kuwa tumeridhikana maelezo haya, tumekubali kulisajili lengo hili. Hivyo inasajiliwa jinsi lilivyo.

Dar es Salaam,
6 Novemba, 1980

J. J. MACKANJA,
Naibu Mwenyekiti,
Mahakama ya Kazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 522

MAHAKAMA YA KAZI

Mkataba wa Hiari Na. 10 wa 1980

baina ya

**JUMUIYA YA WAFANYAKAZI TANZANIA
(JUWATA)**

na

TANZANIA FOOD CORPORATION ARUSHA

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania (JUWATA) na Tanzania Food Corporation Arusha, uliletwa mbele ya Mahakama ya Kazi (Permanent Labour Tribunal) na

Kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Mahakama hiyo, kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (b) na kwa makubaliano ya pamoja na Washauri wa Mahakama (Assessors), Mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa ukiwa na mabadiliko yaliyokubaliwa na pande zote mbili.

Kibali hiki kitaanzia siku ya kwanza ya mwezi Agosti, 1980 na utaendelea kwa muda usiopungua miezi 24.

KUMBUKUMBU YA MKATABA WA HIARI

baina ya

JUMUIYA YA WAFANYAKAZI WA TANZANIA (JUWATA)

na

TANZANIA FOOD CORPORATION LIM.TED—ARUSHA

1. Makubaliano:

Sisi Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania, tujulikanao kwa jina "JUWATA", tunathibitisha kwa maandishi na kwa kuweka sahihi zetu kuonyesha kuwa, kwa uhuru na hiyari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo yahasuyo hali za kazi na mishahara.

2. Hali nyingine za kazi:

Hali nyingine za kazi zitaendelea kutambuliwa kama zilivyo, isipokuwa vifungu Namba 3, 4, 7, 9, 10 vya mkataba Namba 80/78 na vifungu Namba 11 (c), 13, vya Mkataba Namba 19/77.

3. Muda na tarehe ya kuanzia mkataba:

(i) Mkataba huu utanza kutumika kuanzia tarehe 1/8/1980 na utaendelea kutambuliwa na kutumika kwa muda usiopungua miezi 24 (ishirini na nne) kifungu cha mishahara kitakuwa kikijadiliwa baada ya mazi 12 baada ya Mwakiri kuonyesha ufanisi wa mazao.

(ii) Katika kipindi cha miezi 12 ya mwanzo, yeyote wa pande mbili hizi atakayetaka kufuta, kubadili kifungu chochote cha mkataba, itabidi kufuata utaratibu uliowekwa kisheria chini ya Sheria Namba 41/1967 ya Mahakama ya Kazi.

4. Likizo:

Kampuni itaendelea kugharamia nauli ya safari wakati wa likizo ya mwaka ya mfanyakazi hadi nyumbani kwake ya kwenda na kurudi yeye pamoja na mke na watoto wake wa kuzaa au Sh. 180/- iwapo mfanyakazi atataka kulipwa hivyo.

5. Vifo na mazishi (7 wa 80/78):

(a) Pamoja na kuipatia ma'iti ya mfanyakazi aliyefariki vitu muhimu vya mazishi kama ilivyo katika mkataba Namba 19/77 Mwakiri ataipatia familia ya mfanyakazi aliyefariki kiasi cha shilingi 4,000/- kama rambi rambi kwa familia ya marehemu.

(b) Mfanyakazi akifiwa na mke/mume wake wa ndoa au mtoto wake wa kuzaa Mwakiri atampatia rambi rambi kama ifuatavyo:—

(Mke mmoja wa ndoa au mtoto aliyezaliwa na mke mmoja wa ndoa).

(i) Mke/mume mmoja wa ndoa Sh. 1,000/-.

(ii) Mtoto wa kuzaa wa mke/mume mmoja wa ndoa Sh. 500/-.

6. Likizo ya dharura (Fungu II (c) Mkataba 19/77):

Likizo ya dharura ya siku 5 itatolewa kwa mfanyakazi wakati akifiwa na Dada/kaka aliyezaliwa naye siku hizo zitakatwa katika likizo ya mfanyakazi ya mwaka.

7. Matibabu (Fungu 13 Mkataba 19/77):

(1) Wafanyakazi na familia zao (mke wa ndoa na watoto wake wa kuzaa) baada ya kuamuliwa na Central Dispensary ya Moshi-Arusha Occupational Health Services kuwa watibiwe katika hospital watakapopendekeza, watatibiwa katika daraja zifuatazo:—

Walio na mishahara kati ya:—

(a) Walio chini ya cheo cha Supervisor daraja la III.

(b) Walio katika cheo cha Supervisor au Foreman daraja la II.

(c) Walio na zaidi ya cheo cha Foreman daraja la I.

(2) Mgonjwa ambaye hakuzidiwa na iwapo imeamuliwa na Central Dispensary kupata matibabu nje ya Arusha atapatiwa nauli pamoja na posho.

Ufanisi wa mazao:

(A) Wafanyakazi hodari:

(a) Tumekubaliana ya kama wafanyakazi hodari watachaguliwa kutoka kila sehemu (section) ya kazi katika Kampuni nzima kumpata mfanyakazi hodari kwa kila sehemu ya kazi. Kati yao mmoja hodari zaidi ya wote atawakilisha kampuni Wilayani (JUWATA).

(b) Wafanyakazi hodari watazawad'wa kama ifuatavyo:—

(1) Mfanyakazi hodari wa sehemu ya kazi atapewa nyongeza 2 za mishahara.

(2) Mfanyakazi hodari mwakilishi Wilayani atapewa nyongeza 3 za mishahara.

(B) Ufanisi wa kazi:

(i) Uchaguzi wa wafanyakazi hodari utasaidia kuingeza ari ya wafanyakazi ya kuzid'isha ufanisi wao wa kazi.

(ii) Vipimo vya ufanisi vitakuwa kama ifuatavyo:—

C (1) Jumla ya Wafanyakazi ...	1978/79	—	135.
	1979/80	—	135.
	1980/81	—	200.
(2) Jumla ya Mtu—Saa ...	1979/79	—	390,400.
	1979/80	—	392,600.
	1980/81	—	536,000.
(3) Jumla ya Mishahara na Marupurupu ...	1978/79	—	220,7825/50.
	1979/80	—	2,627,228/55.
	1980/81	—	3,610,100/90.
(4) Mazao yaliyotengenezwa.	1978/79	—	kgs. 1,029,8847.4.
	1979/80	—	kgs. 995,615.8.0
	1980/81	—	kgs. 6,684,84.0
Thamani yake ...	1978/79	—	15,385,168.00.
	1979/80	—	21,431,357.00.
	1980/81	—	43,016,100.00.
(5) Wastani wa Mazao kwa Siku ...	1978/89	—	kgs. 3,578.0 thamani Sh. 54,947.02.
	1979/80	—	Kgs. 3,555.8 thamani Sh. 76,540.56.
	1980/81	—	Kgs. 2,387.4 thamani Sh. 153,628.92.
(6) Kila mtu saa iliyotengenezwa mazao ...	1978/89	—	1:2.8. Kgs.
	1979/80	—	1:2.5. Kgs.
	1980/81	—	1:12.5 Kgs.

- C (7) Kila Sh. ya Mshahara marupurupu ilivyozali-sha ... 1978/79 — 1:6/97.
1979/80 — 1:8/16.
1980/81 — 1:11/92.
- C (8) Ongezeko la Ufanisi ... 1979/80 — 3:7% ukilingani-sha 1:1978/79.
1980/81 — 67.1% Ukilinganisha 1979/80.

(a) Viwango vya mishahara:

Viwango vya mishahara tazama kielelezo "A".

Mkataba huu umetiliwa sahihi hii leo tarehe 20 Agosti 1980.

Kwa niaba ya:
Tanzania Food Corporation

N. D. MAMBO,
Meneja Utawala

M. N. KAAYA,
Afisa Maslahi

Kwa niaba ya:
(JUWATA)

G. P. NYINDO,
Katibu wa Mkoa

P. R. MESAWA,
Afisa Mtafiti na Tija

G. E. NJIDILLE,
Katibu wa Wilaya

V. E. MOLLEL,
Mwenyekiti wa Tawi

J. J. M. MACKANJA,
*Naibu Mwenyekiti.
Mwakama ya Kazi*

Arusha.
3 Desemba, 1980

NYONGEZA "A"

VIWANGO VYA MISHAHARA NA MADARAKA YA KAZI

Ngazi	Viwango vya Mishahara	Kazi	Jifa za Kazi
S.1	480/- x 30/- —720/-	Cutter III Wrapper III Packer III Messenger III Assistant Fitter Stores Attendant Cleaner	Anayejua kusoma na kuandika au aliyemaliza shule ya msingi na kufikia darasa la 7.
		Cutter II Wrapper II Packer II Messenger II	Waliomaliza darasa la 7, na Ujuzi wa kazi si chini ya miaka 2 au kupandishwa toka ngazi S.1 baada ya kuonyesha bidii na uhodari wa kazi.
		Mixer Gr.III	Walio na elimu ya darasa la 7 na ufahamu wa hesabu za mwanzo za kujumlisha na kutoa wakiwa na Afya nzuri.
S.2	550/- x 30/- 640/- x 35/- 920/-	Clerical Assistant	Waliomaliza kidatu cha 4 na ufahamu sahihi wa Kiingereza na hesabu.
		Cook Gr. III	Wanaojua kusoma na kuandika na ujuzi wa kazi za upishi si chini ya miaka 2.
		Apprentices	Elimu ya darasa la saba na mahudhurio ya shul- ya ufundi (Vacational Training).
S.3	620/- x 35/- 720/- x 40/- 1,040/-	Mixer Gr. II	Elimu ya darasa la 7 na ujuzi wa kazi ya kuchanganya madawa na vyakula si chini ya miaka 3 au kidatu cha nne na ufahamu mzuri wa Kiingereza na hesabu.

Cutter Gr. I Ujuzi wa kazi miaka 3
Packer Gr. I pamoja na uzoefu wa
Wrapper Gr. I kuendesha machine.
Packer/Wrapper uzoefu
wa kazi si chini ya miaka
3.

Accounts Elimu ya darasa la 7 na
Clerks III ujuzi wa kazi, katika
Sales Clerk III kuandika vitabu vya
mahesabu (Accounting).

Messenger Gr. I Elimu ya msingi na kufikia
darasa la 7 na ujuzi wa
kazi miaka 6 katika
utaratibu wa kazi za
kuendesha ofisini kuweza
kufanya kazi ndogo
ndogo za ukarani.

Cook Gr. II Elimu ya darasa la 7 na
aliyechukua somo la
maarifa ya nyumbani au
ujuzi wa kazi za upishi
miaka 5 katika kuwa-
hudumia wafanyakazi
wanaozidi 200.

Fitter III Darasa la saba na ujuzi
katika kazi za kiufundi
si chini ya miaka mitatu.

Security, Elimu ya darasa la 7 au
Guard Gr. III iliyolingana nayo, ujuzi
na ufahamu wa kazi za
kiulinzi miaka 3 pamoja
na kupata mafunzo ya
awali ya mgambo.

S.4 750/- x 40/-
850/- x 45/-
1,220/- Mixer, Gr. I Waliopandishwa toka
daraja la II baada ya
kuonyesha uhodari na
ujuzi wa kazi zaidi ya
miaka 3, au walioma-
liza kidatu cha nne na
kufanya vizuri katika
somo la sayansi na ujuzi
wa kuchanganya ma-
dawa na vyakula

Machine Kupandishwa toka Cutter
Operator IV I au walio na kidatu
cha nne na ujuzi wa
kuendesha mashine si
chini ya miezi 6.

Accounts Waliomaliza kidatu cha nne
Clerk, Gr. II walio na ujuzi wa utu-
nzaji vitabu vya hesabu
Sales Clerk, au kupandishwa toka
Gr. I A/Clerk III/Sales Clerk
II baada ya kuonyesha
uhodari wa kazi si chini
yamiaka 3.

Typist, Gr. III Elimu ya msingi darasa la 7
Telephone ujuzi wa kazi za kupiga
Operator, Grade taipu kasi ya maneno 40
kwa dakika, waliojifunza
huduma za simu katika
chuo kinachotambulika.

Cook, Gr. I Kupandishwa toka Cook
Gr. II baada ya kuonye-
sha uhodari wa kazi,
Ujuzi wa kazi si chini ya
miaka 7 wa kuwapikia
wafanyakazi zaidi ya 30
na cheti cha Upishi kina-
chotambulika.

Security Guard Kupandishwa toka Gr. III
Gr. II baada ya kuonyesha uho-
dari na ufahamu wa kazi

S.4 750/- x 40/- 850/- x 49/- -1,220/-	Accounts Clerk, Grade II Sales Clerk, Grade I	Waliomaliza kidato cha nne walio na ujuzi wa utunzaji vitabu vya hesabu au kupandishwa toka A/Clerk III/Sales Clerk II baada ya kuonyesha uhodari wa kazi si chini ya miaka 3.	Machine Operator, Grade II	Kupandishwa toka Machine Operator, Grade III na kuwa na uwazo wakundesha mashine aina mbili bila ya msaada na aliye-tumikia daraja hilo zaidi ya miaka 2.
	Typist, Grade III Telephone Operator, Grade.	Elimu ya msingi darasa la 7 ujuzi wa kazi za kupiga taipu kasi ya maneno 40 kwa dakika, waliojifunza huduma za simu katika chuo kinachotambulika.	Account Assistant, Grade II Stores Assistant, Grade II Sales Assistant, Grade I	Waliomaliza kidato cha nne walio na vyeti vya NABE II NABOCE RSA II.
	Cook, Grade I	Kupandishwa toka Cook, Grade II baada ya kuonyesha uhodari wa kazi, Ujuzi wa kazi si chini ya miaka 7 wa kuwapikia wafanya kazi zaidi ya 300 na cheti cha Upishi kinachotambulika.	Typist, Grade I Telephone Operator, Grade I	Kupandishwa toka Typist Telephone Operator, Grade II baada ya kutumikia-daraja hilo si chini ya miaka 3.
	Security, Guard	Kupandishwa toka, Grade III baada ya kuonyesha uhodari na ufahamu wa kazi.	Driver, Grade I	Walio na leseni daraja C na kufanya kazi hiyo bila ya ajali zaidi ya miaka 7.
	Nursing Assistant, Grade II	Waliomaliza kidato cha nne na kupata mafunzo ya uuguzi miaka 2 au kufanya kazi za uuguzi zaidi ya miaka minne na elimu ya darasa la saba.	Assistant Security, Officer, Grade II	Kupandishwa toka Security Guard Grade I, baada ya kutumikia cheo hicho sioi chini ya miaka 3. Waliofika kidato cha nne na kufikia cheo cha Afisa wa Jeshi au Polisi.
	Fitter, Grade II	Kupandishwa toka Fitter III baada ya kuonyesha uhodari wa kazi, au waliofanya kazi hiyo zaidi ya miaka 5.	Trained Nurse	Waliomaliza masomo ya Uuguzi katika Chuo kinachotambulika na anaye kuwa amefanya kazi miaka 2.
S.5 890/- x 45/- 985/- x 50/- -1,385/-	Production Technician, Grade II.	Kupandisha toka Mixar III baada ya kuonyesha uhodari wa kazi, au waliofanya kazi si chini ya miaka 3. Vijana waliomaliza kidato cha 4 na kufaulu vizuri.	Technician, Grade III	Kupandishwa toka Fitter Grade I walio na vyeti vya ufundi daraja la III (Gov. Trade Test).
	Machine Operator, Grade III	Kupandishwa toka Machine, Operator, Grade IV kwa kuonyesha uhodari na ujuzi wa kazi zaidi ya miaka 3 katika kuendesha machine.	Quality Controller, Grade III	Waliomaliza kidato cha 6 na kushinda katika masomo ya sayansi na walio na ujuzi wa Takwimu kavika shughuli za uzalishaji pamoja na uzoefu wa kazi hiyo si chini ya miaka 2.
	Accounts Clerk, Grade I, Store Assistant Assistant Grade II.	Waliomaliza kidato cha nne na kuchukua masomo ya kazi hiyo aliyefaulu utunzaji vitabu NABE I.	Machine Operator, Grade I	Walio na ujuzi wa kuendesha mashine aina yo yote kiwandani. Walio na ujuzi kama Operator Grade II si chini ya miaka 2.
	Typist, Grade II Telephone Operator, Grade II.	Walio na elimu ya msingi na ujuzi wa kazi za kupiga taipu kasi ya maneno 50 kwa dakika. Ujuzi wa kazi za Operator si chini ya miaka 5. Au kupandishwa toka Typist/Operator, Grade III baada ya kuonyesha uhodari wa kazi hizo.	Supervisor III	Walio na sifa za kuongozai na kusimamia kazi, pamoja na kufahamu kazi za Mashine Operators Mixer, Cutter, Packer na Weapper.
	Driver Grade II	Awe na leseni daraja C na kufanya kazi ya udereva bila ajali miaka 5.	Accounts Assistant, Grade I	Walio na uzoefu wa kazi hiyo zaidi ya miaka 3 na vyeti vya NABE II, NABOCE au RSA II.
S. 1,010/- x 50/- 1,160/- x 60/- 1,640/-	Production Technician, Grade I	Kupandishwa toka Production Technician, Grade II baada ya kutumikia daraja hilo si chini ya miaka 3.	Sales Officer	Wenye Diploma katika mambo ya Uuzaji na uzoefu wa kazi chini ya miaka 3.
			Personal Secretary, Grade III	Wenye elimu ya kidato cha nne, ujuzi wa hati mkato kasi ya maneno 80 kwa dakika na kupiga taipu kasi ya maneno 50 kwa dakika. Typist Grade I aweza kupandishwa katika daraja ili

	Transport Officer	Mwenye leseni C na ambaye amekuwa Dereva Grade I si chini ya miaka 3.			Quality Controller, Grade I	Shahada ya Chuo Kikuu hati kazi inayofanana nayo. Kupandishwa toka Quality Controller, Grade II baada ya kutumikia chini ya miaka 5.	
	Assistant Security Officer, Grade I	Kupandishwa cheo toka Grade II baada ya kutumikia sio chini ya miaka 3 Maofisa katika Jeshi/Polisi watafaa katika ngazi hii.			Assistant Accountant, Grade I	Walio na vyeti vya NAB I RSA III na uzoefu wa kazi sio chini ya miaka 3.	
	Staff Nurse	Waliohitimu katika ngazi ya Staff Nurse kama ilivyo serikalini na kuwa amefanya kazi hiyo si chini ya mwaka 1.			Stores Officer Grade I	Materials and Stores Management II.	
	Technician, Grade II	Walio na vyeti vya Ufundi vinavyotambulika serikalini, daraja la II, na kufanya kazi si chini ya miaka 7.			Zonal Sales Representative, Grade III	Walio na Elimu si chini ya kidato cha nne na ujuzi wa kazi kama Sales Representative miaka 3.	
S.8	1,610/- x 80/- 1,850/- x 95/- 2,450/-	Quality Controller, Grade II	Kupandishwa toka Quality Controller, Grade II baada ya kutumikia si chini ya miaka 3 na anayeweza kusimamia kundenisha shughuli Quality Controller bila ya msaada.		Administrative Assistant, Grade II	Walio na Elimu ya kidato cha 6 kupandishwa toka Admn/Assistant, Grade III baada ya uzoefu wa kazi zaidi ya miaka 3. Walio na uwezo wa kazi ya kiutawala na kuzifanya kazi hizo bila ya kulegalega hata kama si kidato cha sita watafikiriwa.	
	Supervisor, Grade II	Kupandishwa toka Supervisor, Grade III baada ya kutumikia si chini ya miaka 2.			Personal Secretary, Grade I	Walio na elimu si chini ya kidato cha Nne na ufahamu sahihi wa Kiingereza na Kiswahili, Ujuzi wa hati mkato kasi ya maneno 100/50 na kupiga taipu kwa dakika walio na ujuzi wa katibu muhtasi si chini ya miaka 5.	
	Assistant Accountant, Grade II, Stores Officer, Grade III	Walio na shahada za NABE MAD I, ASA III Materials of Stores Management II.			Security Officer, Grade I	Kupandishwa kazi toka Security Officer, Grade II baada ya kutumikia si chini ya miaka 3. Maofisa wa Jeshi/Polisi katika cheo cha Superintendent watafikiriwa.	
	Sales Representative	Walio na Elimu kidato cha Nne na amefanya kazi za Uuzaji si chini ya miaka 5.			Foreman, Grade II	Walio na Government Trade Test, Grade I na ujuzi wa uzoefu wa kazi usiopungua miaka 10.	
	Administrative Assistant, Grade III	Walio maliza kidato cha nne na ujuzi wa kazi za kiutawala si chini ya miaka 5 pamoja na ujuzi katika kazi za uhusiano na wafanyakazi pamoja na sheria za Wafanyakazi.			Purchasing Officer	Walio na diploma ya materials Management II au shahada ya Institute of Purchasing and supply inayotambuliwa.	
	Personal Secretary, Grade II	Kupandishwa toka P/S, Grade III, walio na Elimu kidato cha nne pamoja na ujuzi wa hati mkato kazi ya maneno 80 kwa dakika na kupiga taipu maneno 40.			Foreman, Grade I	Kupandishwa toka Foreman, Grade II baada ya Uzalishaji zaidi ya miaka 5.	
	Security Officer, Grade II	Kupandishwa toka S/O Grade III, walio na Elimu ya kidato cha nne na kazi za uongozi wa kazi za kiulini si chini ya miaka 5 au maofisa wa Jeshi/Polisi waliofikia ngazi ya Inspector.		S.9	2,895/- x 130/- 2,995/- x 150/- 4,195	Accountant, Grade II	Walio na shahada ya NAD I AND II na ujuzi wa kazi si chini ya miaka mitatu.
S.8	1,610/- x 80/- 1,850/- x 95/- 2,450/-	Technician, Grade I	Walio na Trade Test, Grade I na au ujuzi wa kazi wa hali ya juu chini ya miaka 7.			Administrative Assistant, Grade I	Kupandishwa toka Admn. Asst. II baada ya kuwa na uzoefu wa kazi hiyo zaidi ya miaka 5 walio na shahada ya Chuo Kikuu katika somo la Uendeshaji wa Makampuni.
S.9	2,100/- x 105/- 2,415/- x 120/- 3,357/-	Foreman, Grade II Supervisor, Grade I	Kupandishwa toka Supervisor, Grade I baada ya kutumikia si chini ya miaka 3 na kuwa na sifa za kuridhisha katika uongozi. Walio na ujuzi katika utengenezaji Biscuits/Pasta si chini ya miaka 7 na kuonyesha uhodari wa kazi katika Supervisor, Grade II.			Marketing Officer, Grade II	Walio na elimu si chini ya kidato cha 6, na ujuzi wa kazi ya Sales Representatives ya Chuo Kikuu katika Elimu ya Biashara
						Sales Promotion Officer, Grade II Zonal Sales Representative, Grade II	

TAARIFA YA KAWAIDA N° 523

MGOGORO WA KAZI

Na. 10 ya 1980

Baina ya

JUMUIYA YA WAFANYAKAZI TANZANIA
(JUWATA)

(Kikimetea mwanachama wao Nd. J. K. Pallangyo)

na

ZAMBIA TANZANIA ROAD SERVICE DAR ES
SALAAM**Mahakama:**J. J. M. MACKANJA, Naibu Mwenyekiti.
J. W. MPANGALA, Mshauri—JUWATA.
M. I. BARKAA, Mshauri—A. T. E.**Kuwakilisha JUWATA:**

Nd. KALUWA—Katibu Mkuu Msaidizi.

Mlalamikaji:

J. K. PALLANGYO, Yupo.

Kuwakilisha Waajiri:J. M. MSANYA, Meneja Maslahi.
A. D. S. KUMWEMBE, Afisa Maslahi.

Kwanza kabisa Mahakama ingependa kusema kwamba licha ya matatizo madogo madogo ya hapa na pale, pande zote mbili zilikuwa zimejitayarisha vema katika mgogoro huu, jambo ambalo limesaidia kutoa nuru ya kutosha katika masuala yanayobishaniwa. Kwa hiyo Mahakama inachukua fursa hii kuwapongeza wote ambao wameshiriki katika kikao hiki hadi kufikia hatua ya kutuwezesha kufika uamuzi wa masuala haya kama tunavyotaka kufanya hivi punde. Sasa tutazame mgogoro huu jinsi ulivyoanza.

Kulingana na hati za mawasiliano zilizofikishwa mbele ya Mahakama, Katibu Mkuu wa JUWATA, kwa mujibu wa k. 4 (1) cha Sheria ya Mahakama ya Kazi, Na. 41 ya 1967, alitangaza mgogoro wa kikazi baina yao na waajiri wa mlalamikaji, M/S Zambia Tanzania Road Service Ltd. (ZTRS), kutokana na kuachishwa kazi Ndugu Pallangyo. Baada ya kupitia ngazi zote za kushughulikia mgogoro wa kikazi kama zilivyowekwa kisheria, hatimaye umefikishwa mbele yetu. Kwa kifupi katika mgogoro huu JUWATA wanadai kwamba kuachishwa kazi kwa Ndugu Pallangyo ni kitendo cha uonevu kwa kuwa hana kosa la kuhalalisha hatua hii. Wanaondelea kudai kwamba Meneja wa Maslahi ambaye alimwachisha kazi hana mamlaka ya kufanya hivyo kwa hiyo amri ya kumwachisha kazi mlalamikaji ni batili kisheria.

Kwa upande wao waajiri wanadai kwamba mlalamikaji alikuwa ni mkorofi, mkaripiaji na mtu ambaye alikuwa hana uhusiano mzuri na wafanyakazi wengine kinyume cha Ibara ya 15 ya Mwongozo wa TANU (1970). Wanadai pia kwamba kukataa uhamisho bila uthibitisho wa daktari ni kitendo cha utovu wa ndhamu. Mlalamikaji alikuwa pia mtovu wa nidhamu (insubordination) alipokataa kutii amri ya mwajiri wake alpokuwa amesimamishwa kazi mara tu kabla ya kuachishwa kazi.

Kwa kuwa mambo haya yanayobishaniwa hayakupata ufumbuzi mbele ya msuluhishi aliyechaguliwa na Kamishna wa Kazi sasa Mahakama hii inao wajibu wa kutoa uamuzi ambao utazibana pande zote mbili kisheria kulingana na mamlaka yake. Ufuatao ndio uamuzi, pamoja na sababu za uamuzi huo, juu ya masuala mbali mbali yanayojitokeza katika ushahidi.

UAMUZI

Tutaanza uamuzi huu kwa kutazama ajira ya mlalamikaji. Suala hili halibishiwi hata kidogo. Kulingana na ushahidi uliotolewa aliajiriwa kama karani kuanza tarehe 6 Februari, 1969. Baadaye alihamishwa kwenye Idara ya Uchukuzi na Usafirishi (Traffic and Freight Department). Mnamo Juni 18, 1970 alihamishwa Mbeya kutoka Dar es Salaam kuchukua nafasi ya Mtaliani mmoja kama Msimamizi (Supervisor). Maadam alikuwa amehamishwa bila barua kutoka Idara ya Utumishi, ilibidi uhamisho huo uthibitishwe kwa maandishi; uthibitisho huo umo katika barua aliyound kiwa na ambayo imetolewa kama kielelezo cha JUWATA na 1 na Na. 3. Kazi hiyo ya usimamizi mlalamikaji alipewa kwa majaribio ya mwezi mmoja. Inaonekana ali mudu kazi hiyo bara bara, kwani mnamo Julai 29, 1970 aliaandikiwa barua ya kumthibitisha kazini (JUWATA Na. 2). Katika barua hiyo pia mlalamikaji alipandishwa cheo kutoka daraja la 4 hadi daraja la 6. Alipandishwa cheo tena tarehe 30 Julai 1970 kuwa Mrakibu wa Usafirishi (JUWATA Na. 3). Alihamishwa tena Dar es Salaam mwaka huo huo na tarehe 11 Desemba, 1970 alipandishwa cheo kuwa Meneja wa Uchukuzi (Traffic Manager) kwa majaribio ya miezi mitatu (JUWATA Na. 4).

Katika mfululizo wa kupewa madaraka, mlalamikaji aliteuliwa kuwa Kaimu Meneja wa Tawi tarehe 6 Desemba, 1974 wakati Meneja wa Tawi alipokwenda Ulaya. masomoni kwa muda wa miezi mitatu (JUWATA Na. 5).

Mlalamikaji alibadilishwa cheo kuwa Company Assistant Operations Manager (JUWATA Na. 6). Kulingana na ushahidi uliotolewa cheo hiki kilikuwa ni kinya na mlalamikaji ndiye alikuwa mtu wa kwanza kuteuliwa kushika wadhifa huo. Kazi hii ilikuwa mpya, hivyo alipewa majaribio yote ambayo angetekeleza kwa maandishi (JUWATA Na. 7).

Hadi kufikia wakati huu ushahidi wa upande wa JUWATA unaonyesha kwamba mlalamikaji alikuwa ni mchapakazi na ambaye alikuwa ana ndhamu ya juu hata akastahili kupandishwa cheo. Lakini picha inayotolewa na waajiri ni mbaya, kiasi kwamba hata kule kumpandishwa yeye ni kama jambo la muujiza. Kama tabia hiyo ni ya kweli mlalamikaji alikuwa hasitahili kuthibitishwa kazini au kupandishwa cheo. Na hasa imedaiwa ifuatavyo. Kwamba mlalamikaji alipohamishwa Mbeya mwaka 1970 alikuta uwelewano mkubwa baina ya wafanyakazi na viongozi wao. Alifakuta watu wengi pale akiwemo Watson Siluwonde, Shahidi wa 1 wa Waajiri, ambaye alikuwa ni karani wake. Mlalamikaji kama msimamizi wa uchukuzi alikuwa pia na ukumu la kuthibitisha na kuidhinisha malipo ya posho na bonasi kwa madereva. Lakini kutokana na tabia yake ya unyapara, ukaripiaji na uzeembe kwa kuchefewa kufika kazini madereva walikuwa wanachelewa kulipwa, jambo ambalo lilikuwa linachelewa kuanza kwa safari. Inaonekana kutokana na mwamko wa kisiasa wafanyakazi hawakuvumilia kuendelea kunyanyaswa. Kwa hiyo Kamati ya Kazi iliamua kuitisha kikao ambacho kilizungumzia tabia ya mlalamikaji. Baada ya kikao hicho Kamati ilimwandikia barua ya tarehe 7 Oktoba, 1970 (Kielelezo cha Uajiri Na. 1). Wafanyakazi walimweleza mlalamikaji mambo haya, kati ya mengine mengi:

"... Ndugu mpenzi utakubaliana nami kwamba kiongozi yeyote anapaswa kuwa mtu wa haki, kwa hiyo ni wajibu wako kulinda haki za kazi halikadhalika haki za ubinadamu kwa uumla..."

Utakubaliana nasi kwamba mpaka sasa idadi kubwa sana za mashtaka katika kiwanda hiki ni toka katika wizara yako, na kuna baadhi ya watumishi ambao mpaka sasa wameisha shinda kuitambua kamati ya kazi hata wameisha vuka mpaka na kukimbilia kwenye siasa..."

Ndugu mpenzi utahumbuka kwamba mizozo katika wizara yako imeishazifikia hata nchi za ng'ambo na kuandikwa katika magazeti, na hili si jambo jema . . .

Mlalamikaji alikana ku pokea barua hii, lakini badaa ya kuchunguza mwenendo wa shahidi huyu mbele ya ushahidi wa shahidi wa pili upande wa waajiri, Yonani Anyimike, na tukitazama kwamba haikuonekana sababu ya kumsingiza, Mahakama inaona kwamba mashtaka haya ni ya kweli. Lakini mambo haya yalitokea miaka kama tisa hivi kabla ya kumwachisha kazi mlalamikaji. Kwa kuwa mlalamikaji hakupewa barua ya onyo au onyo la maneno ya mdomoni, Mahakama inaona kwamba ingawa tabia ya mlalamikaji ha'kuridhisha hakusitabili onyo. Onyo tu la wakati huo (MWAJIRI Na. 6) linahusu mambo tofauti kabisa. Aidha mambo haya ni zamani mno kwamba huyaweka kama makosa ya kusababisha adhabu kwa sasa si jambo la busara. Ila inatosha kusema kwamba ushabidi huo unaonyesha tabia ya mlalamikaji ali poanza kupewa madaraka.

Menejimenti wametoa madai mengine kwamba tabia hiyo mbaya mlalamikaji alikuwa nayo hata alipoteuliwa kuwa Kaimu Meneja wa Tawi. Imedaiwa kwamba tatizo kubwa la mlalamikaji lilikuwa ni kitokuwa na mwamko wa kisiasa kama aivyosema Ndugu Mfaume Yusufu (Shahidi wa 5 wa upande wa waajiri).

Naye Shahidi wa 4 wa upande wa waajiri, Marko Salehe, amesema kwamba wakati yeye na mlalamikaji walipokuwa eneo moja la kazi wakifanya kazi ambazo zilikuwa z kibusiana, mlalamikaji alijenga tabia ya kutoshirikiana na wenzake. Hali ilikuwa mbaya hasa mlalamikaji alipopandishwa cheo kuwa Meneja wa Uchukuzi (Traffic Manager). Alikataa hata kutoa ushauri na maelekezo kwa wale waliokuwa chini yake. Mahakama ilikuwa imeyapa maelezo haya uzito kabla ha'ahojiwa na upande wa JUWATA. Baada hoja hizo imebainika kwamba kutokana na mapendekezo ya mlalamikaji kama Meneja wake, shahidi huyu alifukuzwa kazi ingawa baadaye alirudishwa baada ya uamuzi wa Baraza la Usuluhishi. Hata kitabia shahidi huyu aliridhika kwamba ushahidi wote wa kishindo ulikusudiwa kulipiza kisasi, jambo ambalo linaweza kupotosha usimamiaji wa haki katika masuala yato kanayo na mgogoro huu. Kwa kifupi Mahakama inasema kwamba shahidi huyu hana ukweli wowote katika maezo aliyoyatoa. Tungekuwa na mawazo tofauti kama watu wengine wangeyathibitisha madai haya.

Imedaiwa kwamba alipokuwa Company Assistant Operations Manager mlalamikaji, bila sababu ya maana alimtukana Patson Sintufya, (shahidi wa 6 wa waajiri), baada ya kumuomba apeleke taarifa ya trailer lililoungua njiani, TZ 2407. Baada ya kuambiwa hivyo mlalamikaji:

"Alijibu kwamba alikuwa mkuu wangu wa kazi kwa hiyo hakuwa tarishi wangu. Akasema huo ulikuwa ni ujinga na kwamba mimi nilikuwa mpumbavu."

Madai haya inasemekana mlalamikaji aliyatoa mbele ya kamati ya UNIP, Chama cha kisiasa kinachotawala Zambia, hata ikabidi viongozi wa UNIP kuandika barua kulalamika (UAJIRI Na. 2). Waandishi wa barua hiyo walimfahamisha mlalamikaji kitabia na mkoloni mmoja aliyeitwa Welensky. Shahidi mwingine kutoka Zambia aliyelalamika kwamba alitukanwa bila sababu ni Donald Chishimba, shahidi wa saba upande wa waajiri. Yeye amedai kwamba alikuwa amfahamu mlalamikaji walipopambana huko Matumbo Mpika. Mlalamikaji alikuwa akiendashwa na Escorter alipowakuta mafundi makanika, akiwemo shahidi huyo wakitengeneza magari eneo ya Matumbo. Wao hawakumuona alipowaita kwa hiyo hawakwenda. Bila kujitambulisha yeye ni nani aliwatukana:

"I am going to fire you, you stupid bastards. Your are just playing around, you don't want to attend to your duties".

Aliondoka kuelekea Mpika na shahidi huyu akaenda kulalamika kwa mkuu wa kazi. Kutokana na hoja za mlalamikaji Mahakama imeridhika kwamba mapambano haya yalitokea. Jambo la ajabu menejimenti haikumuonya mlalamikaji, au kumtaka ajieleze, kuhusu matukio haya. Walakini kwa kuwa matukio yenyewe yanazidi ya miezi sita inaonyesha kwamba walipuuzwa. Kama waliyapuuzwa hawezi kusikika sasa wakimlaumu mlalamikaji. Inawezeke na kwa kujenga tabia ya kutojali matukio haya menejimenti ilimpa mlalamikaji moyo wa kujihusisha na tabia hii ambayo inanekana ilizidi kuota mizizi. Lakini kama tulivyo sema awali, makosa haya sasa hayawezi kuwa msingi wa kumchukulia hatua licha ya kutoa mwanga jinsi mlalamikaji alivyojenga tabia ambayo sasa inalalamikiwa. Ingawa mlalamikaji alikuwa akijihusisha na makosa haya inaonekana alikuwa akiifanya kazi yake vizuri hata kusitabili kupandishwa cheo mara kwa mara. Tutaona baadaye kwamba hata uhamisho uliosababisha mgogoro huu ulimuangukia mlalamikaji kutokana na uwezo wake wa kufanya kazi. Alipotoa sababu ya kutotekeleza amri ya uhamisho wake kuwa alikuwa akipata matibabu Muhimbili aliuchimbia utumishi wake kaburi. Huo ndio ulikuwa mwisho wa safari ya utumishi ambao umebainisha misukusuko mingi ambayo ilikuwa haijulikani nje. Tutalichunguza suala hili kwa kujumlisha vipengere vyote vinavyohusiana, hasa ajali zilizomletea madhara ya mwili.

Alipokuwa Traffic Manager mnamo Oktoba 9, 1975 alipata ajali akaumia mguu wa kushoto uliipasuka goti, wakati akitoka ndani ya gari nyumbani kwake. Baada ya hapo alitibiwa katika Shirika la Afya Muhimbili hadi Januari 7, 1976 siku ambayo alipelekwa kupata matibabu kwenye Idara ya mazoezi ya viungo: Physio-Therapy Department. Tarehe 11 Aprili, 1978 akapata ajali nyingine akaumia mguu wa kulia baada ya kuanguka alipokuwa akitengeneza vioo vya nyumba yake. Kutokana na madhara ya mwili aliyopata mlalamikaji aliendelea kupata matibabu akiwa mgonjwa wa kutibiwa na kurudi nyumbani. Alishauriwa kuendelea na mazoezi ya viungo hadi hapo ambapo angepona. Wakati akitibiwa alikuwa akiendelea na kazi kama kawaida ingawa hakuwa na "sick-sheet". Kwa kuwa hakuwa na "sick-sheet" sasa menejimenti inadai kwamba haikuwa na taarifa rasmi ya matibabu ya mlalamikaji. Kwa hali ya sheria na kanuni za kazi zilivyo nchini ni jukumu la mlalamikaji kutoa uthibitisho. Hali hii inatokana na taarifa ya Serikali Na. 152 ya 1972 ambayo inasema:

"(b) Sick Leave; ...

(i) ...

(ii) ...

(iii) Any employee falling ill should make every effort to notify his employer at once and the employer shall, if possible, issue him with a sick-sheet."

Japokuwa mlalamikaji hakuwa na hati ya matibabu kutoka kwa mwajiri (sick-sheet) kila alipokuwa anakwenda kutibiwa Muhimbili, upo ushahidi (Mwajiri Na. 24) unaoonyesha kwamba waajiri waliyafahamu madhara ya mwili aliyoyapata mlalamikaji kabla ya kupewa uhamisho wa kwenda Iringa. Ushahidi huo ni hati ya mkono iliyoandikwa na nganga wa Kampuni ya tarehe 13 Aprili, 1978, yaani kielezo hicho cha Mwajiri Na. 24, ambayo kwayo Casualty Department ya Muhimbili iliombwa kumhudumia mlalamikaji madhara aliyopata Aprili 11, 1978. Lingekuwa jambo tofauti kama waajiri wangedai kwamba hawakujua kama mlalamikaji alikuwa hajapona alipohamishiwa Iringa.

Kulingana na madai ya JUWATA inaonekana kwamba mlalamikaji alikuwa bado hajapona sawa sawa Kampuni alipoandaa semina huko Mbeya. Taarifa ya semina hiyo ilitawanywa kwa viongozi wote waliotakiwa kushiriki, akiwemo Ndugu Pallangyo, ambaye alikuwa Assistant Operations Manager—Dar es Salaam. Hii taarifa ilitolewa kwa mujibu wa kielelezo cha mwajiri Na. 12. Semina

ingefanywa tarehe 25 na 26 Januari, 1979. Wakati huo huo mlalamikaji aliomba likizo kuanzia tarehe 9 hadi 24 Januari, 1979. Katibu Meneja Mkuu, Ndugu Maskini (Shahidi wa Mwajiri Na. 8), aliyeidhinisha likizo hiyo alisema kwamba alifuta idhini yake ili mlalamikaji aende kuhudhuria semina kwanza. Madai hayo yanatokana na maandishi haya kwenye fomu ya maombi ya likizo: "Wait until the seminar at Mbeya is over". Mlalamikaji alidai kwamba angerudi mapema ili ahudhuria semina hiyo. Baada ya uthibitisho huo Naibu Meneja Mkuu alifuta maneno ambayo nimeyanakili hapo juu kulingana na kielelezo cha JUWATA Na. 8 na kielelezo cha Mwajiri Na. 13.

Mlalamikaji ameyapinga madai haya kwa kusema kwamba yeye hakuarifiwa kwenda kuhudhuria semina. Baada ya kutazama hati hizi mbili mimi naona kwamba haupo ushahidi wa kuonyesha kwamba mlalamikaji anasingiziwa katika jambi hili. Na hata kama hakuarifiwa, alitakiwa kurudi ofisini kabla ya semina kuanza.

Vyo vyote iwavyo, semina iliendelea kama ilivyokuwa imepangwa. Naibu Meneja Mkuu ameambia Mahakama kwamba wajumbe walitazamia kwamba yafanywe mabadiliko ya uongozi. Katika kutekeleza maazimio hayo Meneja Mkuu aliandika barua (Mwajiri Na. 14) akiagiza kwamba viongozi watatu wabadilishwe kazi; (a) Bwana W. T. Scous aliyekuwa Workshop Manager awe Road Technical Manager; (b) Bwana G. R. Kamat aliyekuwa Technical Engineer awe Acting Technical Manager; (c) Bwana J. K. Pallangyo aliyekuwa Assistant Operations Manager aende Iringa kuwa Outstations Superintendent badala ya Bwana C. Chezzy ambaye angechukua nafasi ya mlalamikaji. Katika kutekeleza agizo hili Meneja wa Maslahi alimwandikia mlalamikaji barua (Mwajiri Na. 15 na JUWATA Na. 9), kwamba alikuwa ameteuliwa kuwa mrakibu wa vituo vya nje na wamba aende huko bila kuchelewa. Tutakavyoona hivi punde, hali ya mambo ilibadilika ghfla baada ya mlalamikaji kupewa uhamisho huu. Bila kusema kwamba hataki kwenda uhamishoni mlalamikaji alisema ilimuwia vigumu kuhama kwa kuwa alikuwa akitibiwa na pia alikuwa na matatizo kadhaa ya nyumbani (JUWATA Na. 10 na Mwajiri Na. 15). Meneja wa Maslahi alijibu akisema kwamba ingawa menejimenti inafikiria kwamba pointi hizo mbili alizotoa mlalamikaji zingeweza kumchelewesha kuhama mara moja, menejimenti ilitaka kujua kwa uhakika ni lini mlalamikaji angekuwa tayari kuchukua nafasi yake Iringa. Meneja wa Maslahi alitaka kusisitiza kwamba kuwepo Iringa kwa mlalamikaji kulikuwa muhimu kwani Kampuni iliona kwamba, katika mabadiliko yaliyotokea, mlalamikaji ndiye peke yake alikuwa ("potential person") mtu wa kumudu kuthibiti vituo vya eneo hili (JUWATA Na. 11). Mlalamikaji alitakiwa kujibu barua hii Kumb. Na. PF/1573/79/nm katika muda wa saa 24 (Mwajiri Na. 15).

Katika majibu yake (JUWATA Na. 12 ambayo pia ni sehemu ya kielelezo cha mwajiri Na. 15) mlalamikaji alisisitiza kwamba alikuwa na matibabu ya mara kwa mara Muhimbili Medical Centre, na kwamba kwa hali hiyo ilimuwia vigumu kujua kwa hakika siku ambayo matibabu hayo yangekoma. Kwa hiyo ilikuwa vigumu kuhama mara moja kabla ya kupata ushauri wa daktari wake. Barua hii iliandikwa Februari 9, 1979.

Kama nilivyosema awali Menejimenti ilikuwa na msiamu kwamba haikuwa na taarifa juu ya ugonjwa na mambo kwamba haikuwa na taarifa juu ya ugonjwa na matibabu ya mlalamikaji. Kulingana na barua yao Kumb. Na. PF/168/1573/79/rm ya 13 Februari, 1979 (ambayo ni sehemu ya kielelezo cha Mwajiri Na. 15 na JUWATA Na. 13), aliambiwa kutoa uthibitisho wa maandishi kama ushahidi wa madai hayo. Baada ya hapo menejimenti ingechukua hatua inayofaa kulingana na mkataba wa ajira baina yao na mlalamikaji. Uthibitisho

huo ulitolewa kwa kuwasilisha barua iliyoandikwa na Therapist. Ndugu Kaaya ambayo ilitolewa kama kielelezo cha Menejimenti Na. 16 na cha JUWATA Na. 14. Barua hiyo iliandikwa kwa yeyote anayehusika ambayo ilionyesha kuwa ilikuwa ni kweli Ndugu Pallangyo alikuwa akipata matibabu ya kucheza viungo. Ndugu Kaaya alitwa kutoa ushahidi katika mgogoro huu kutoa nuru zaidi juu ya barua hiyo.

Ndugu Kaaya alisema hapa Mahakamani kwamba mlalamikaji alihamishiwa kwake kutoka Orthopaedic Department tarehe 7 Januari, 1976 kutibwa "Tibia with tear of medical meniscus". Ili kuondoa uvimbe alitibiwa kwa "infra red rays". Goti lilikuwa limevimba $2\frac{1}{2}$ cm zaidi ya goti la kulia lililokuwa zima. Alipofanyiwa "review" tarehe 5 Februari, 1976, alionyesha kwamba alikuwa akiendelea kupata nafuu. Alipewa ushauri wa kuacha matibabu kwa muda wa miezi mitatu. Mlalamikaji hakurudi tena hospitali hadi baada ya miezi mitano, yaani Julai 9, 1976, aliposema kwamba tatizo lake wakati huo lilikuwa ni kupata maumivu wakati wa baridi au akitembea muda mrefu. Alishauriwa kufunga bandage asikiapo maumivu nyakati za baridi. Mlalamikaji alirudi hospitali tarehe 24 Juni, 1977 kwa ajili ya maumivu hayo hayo. Baada ya kupimwa alionekana ana uvimbe na maumivu. Hivyo alianziswh tena matibabu ya "ultra sonic waves" na alisheuriwa arudi baada ya majuma matatu. Aliporudi tarehe 22 Julai, 1977 alionyesha maendeleo hivyo akatibiwa kwa "infra red rays" peke yake.

Tarehe 17 Aprili, 1978 mlalamikaji alianguka akarudi hospitali akilalamika kwamba ameumia mguu wa kulia na kifua. Aliendelea na matibabu yake tarehe 3 Mei, 1978; tarehe 12 Aprili, 1979 alivutwa maji kutoka kwenye goti la kulia na kupewa mapumziko hadi tarehe 18 Aprili, 1979, n.k. Jambo la muhimu ni kwamba alipohojiwa shahidi huyo alisema kwamba mlalamikaji angepata matibabu katika hospitali za K.C.M.C. Moshi, Bugando ya Mwanza na Tanga. Maoni haya, tutakavyoona yanapingwa na taarifa ya Mkurugenzi wa Idara ambayo inajumuisha Physio-Therapy Department. Alipoulizwa kama matibabu yangemzuia mlalamikaji kuhama alisema hapana. Iwapo angeombwa kufanya hivyo. Menejimenti haikumboa hivyo, lakini kwa vile barua hiyo haikusema mlalamikaji hawezi kuhama, walimsimamisha kazi mara moja. Hata hivyo inatosha kujiridhisha kwamba menejimenti ilikwishapata taarifa ya matibabu kabla ya kuandika barua ya kumsimamisha kazi mlalamikaji (JUWATA Na. 15 na Mwajiri Na. 18).

Katika barua hiyo mlalamikaji alitakiwa kupiga ripoti saa 1.30 asubuhi na 8.00 alasiri kila siku isipokuwa Jumapili na sikukuu za kitaifa kwa Assistant Superintendent of Security. Menejimenti hawakuwambia kwa nini afanye hivyo na taarifa atoe kwa mtu ambaye Ndugu Kaluwa amesema alikuwa chini yake kimadaraka badala ya Naibu Meneja Mkuu ambaye ndiye alikuwa mkuu wake wa kazi. Naibu Meneja Mkuu alipoulizwa Mahakamani alisema kwamba ilibidi kutoa agizo hilo ili kusubiri mipango ya kumpeleka mlalamikaji kupimwa hospitali ikamilike. Nimefikiria sana ushahidi huu na nimeona haikuwapo sababu iliyomzuia Meneja wa Maslahi kusema hivyo wazi wazi katika barua ya kumsimamisha mlalamikaji. Ingawa nia ya kufanva hivyo ilikuwa ni njema lakini kitendo chenyewe ni cha usumbufu. Sarti la aina hiyo linaweza kueleweka kama kosa ni la jina na upo wasi wasi kwamba mshtakiwa anaweza kutoroka. Kama menejimenti iliona umuhimu wa kumpima mlalamikaji, basi haipo sababu ya maana kwa kumsimamisha kazi kabla ya wakati huo. Vile vile yalikuwa ni makosa kwa upande wa menejimenti kumtaka mlalamikaji kuripoti kwa mtu ambaye alikuwa chini yake kimadaraka.

Makosa hayakuwa upande wa menejimenti peke yake. Baada ya kupokea barua ya kusimamishwa kazi mlalamikaji aliandika barua ambayo ni ushahidi wa chuki na kiburi, ambavyo ni viini vya utovu wa nidhamu. Barua hiyo (Mwajiri Na. 19) inasema kwamba maadamu Naibu Meneja Mkuu alishindwa kuthibitisha ulazima wa mlalamikaji kupiga ripoti mara mbili aliamua kuvunja agizo hilo la bandia. Ukweli ni kwamba agizo hilo halikuwa la bandia, lilikuwa halisi; na alipolivunja aliachishwa kazi mara moja. Kabla ya hapo mlalamikaji alikuwa amedai kupewa sababu zilizofanya asimamishwe kazi (barua hii ni sehemu ya Mwajiri Na. 19 na JUWATA Na. 17).

Alipoachishwa kazi, kulingana na kielelezo cha Mwajiri Na. 20 na cha JUWATA Na. 18, mlalamikaji alielezwa kwamba maadam barua kutoka Muhimbili Medical Centre haimkatazi kuhama, kukataa kwenda Iringa kilikuwa ni k'tendo cha utovu wa nidhamu (insubord nation) kiasi cha kuvunja mkataba wa ajira yake. Aliachishwa kazi na kutakiwa kuchukua haki zake kutoka kwa Mhasibu Mkuu. Ingawa mlalamikaji alipewa barua hii yeye aliandika barua ya kejeli akidai kwamba kuachishwa kwake kazi kulikuwa batili na kwamba kitendo hicho ni cha kuchekesha! (JUWATA Na. 19 pamoja na Mwajiri Na. 21).

JUWATA wanapinga hatua ya menejimenti ya kumwachisha kazi kudai kwamba Meneja wa Maslahi hana mamlaka ya kufanya hivyo. Katika ngazi aliyokwishafikia mlalamikaji mamlaka yenye uwezo za di yangehusika. Kuhusu suala hili menejimenti wamedai kwamba Meneja wa Maslahi ni kati ya viongozi ambao wamepewa mamlaka ya nidhamu kwa wafanyakazi na kwamba kati ya wote Meneja Mkuu ndiye ngazi ya mwisho. Yeye Meneja Mkuu anaweza kuamuru, baada ya kuridhika kwamba mfanyakazi amekosa, afukuzwe au aachishwe kazi. Msimamo wa menejimenti haukutaja kama ni jambo la muhimu kumpa mfanyakazi nafasi ya kujitetea kwa maandishi au kwa maneno ya mdomoni kabla ya kuachishwa au kufukuzwa kazi. Katika mgogoro huu nafasi hiyo haikutolewa ili mlalamikaji ajieleze kwa nini asichukuliwe hatua ya kuachishwa kazi aliposhindwa kutoa uthibitisho wa matibabu ambao ungeiridhisha menejimenti. Tukiyachunguza maelezo ya menejimenti kwa undani zaidi tunaweza kujiridhisha kwamba wao wanaona wanayo haki ya kuajiri na kufukuza au kuachisha kazi wapendavyo ilimradi tu wameridhika na makosa ya mfanyakazi.

Kwa Kiingereza tungesema wanaona wana "prerogative and the right to hire and fire" kuhusu mtumishi ye yote yule na wakati wo wote. Hali hiyo ni ya hatari na wala haipo hapa nchini kisheria Mahakama inavyofahamu ni kwamba katika kila mkataba wa ajira panakuwa na sharti (warranty) ambalo wajibu wa kufanya kazi wa haki ya kulipwa ujira labda kama itakuwa haiwezekani kuendelea na mkataba huo. Hali ambayo itaweza kusababisha kuvunja mkataba ni pamoja na mambo yasiyozuilika kuingilia kazi (yaani frustration of the performance of the contract) kama vile kufilisika kwa mwajiri; maradhi yasiyotibika au ya kujitakia mwenyewe kwa upende wa mwajiriwa; kuharibu mali ya mwajiri; utovu wa nidhamu mahali pa kazi; kufungwa gereza kwa ajili ya makosa ya jinai; pamoja na mambo mengine yahusianayo nayo. Hata kama hali ya mambo imekuwa hivyo mfanyakazi anayo haki ya kujitetea kabla ya kuchukuliwa hatua yo yote. Hii ni haki ya asili ambayo nchi yetu inaitambua kisheria. Vinginevyo uendeshaji wa masuala ya utumishi ungekuwa ni wa kisultani, wa kuwadhibu walio na makosa na wale wasio na makosa mradi tu menejimenti inona imejiridhishwa. Ingawa Mahakama hii imezungumzia suala hili karibu kila mgogoro uliofikishwa mbele yake, tutazidi kusema hivyo mpaka hapo waliobahatika kuwa na wadhifa wa kuongoza watakapotambua makosa yao na kukubali hali halisi ilivyo. Msimamo huu unayahusu hata mashirika na makampuni ya nje yanayoe-

ndesha shughuli zao hapa kwa kuwa yanawajibu wa kutii na kutenda kulingana na utashi wa sheria za nchi. Kwa hiyo ninasema kwamba kwa kumnyima mlalamikaji haki yake ya kujitetea uamuzi wa menejimenti unakuwa ni batili kisheria. (Tazama I. H. MAHONA v. UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM, High Court (DSM) Civ. Case Na. 83 of 1977). Inatosha kwa wakati huu kusema kwamba suala hili litazamwe pamoja na utaratibu uliofutatawa katika kumchukulia mlalamikaji hatua.

Kwa upande mwingine menejimenti wamedai kwamba mlalamikaji alikuwa akitumia vibaya magari ya kampuni. Kwa muda aliofikia madaraka ya kupewa usafiri na kampuni mlalamikaji aliharibu magari yapatayo matano jambo ambalo liliiletea kampuni gharama bure katika kulipa matengenezo. Aidha, kutokana na tabia yake ya kuto-shirikiana na wenzake alitoa taarifa ambazo hazikuwa za kweli kumhusu Naibu Meneja Mkuu kuhusu fenicha na gari alililonunua kihalali kutoka kwenye Kampuni.

Ingawa jumla ya watumishi 70 walikuwa wamezuwa magari na kampuni, akiwemo Ndugu Maskini, Ndugu Pallangyo alitoa taarifa kwa Kikosi cha Kuzuia Rushwa kumhusu Ndugu Maskini juu ya ununuzi huo. Kama jambo hili ni kweli basi wanaohusika walilipuza kwani hakuna hatua yo yote iliyochukuliwa kulifuatilia. Wakini haukupatikana ushahidi wa kulithibitisha. Katika msukumo mwingine wa visa dhidi ya viongozi wenzake inadaikiwa kwamba mlalamikaji alitoa malalamiko ya uwongo mbele ya polisi kwamba Ndugu Msanya alimwambia kitabu chake cha kumbukumbu zikiwemo Sh. 8,000/- taslim, malalamiko ambayo yalimletea msukusuko Ndugu Msanya bila ukweli wo wote (Tazama kielelezo Mwajiri Na. 28). Tabia ya namna hiyo haiwezi kudumisha uhusiano kazini kwa hiyo ni lazima ilaaniwe, kwani bila uelewano kazini, hasa baina ya viongozi, tutakuwa tunajidanganya kuwategemea wafanyakazi wa kawaida kuwaheshimu viongozi wao. Kuhusu kuharibu magari Mahakama inaona kwamba hatua iliyochukuliwa na menejimenti ya kumuonya mlalamikaji ilikuwa inafaa kabisa. Lakini kwa kuwa menejimenti ilitaja tu kama sababu ya kumwachisha kazi mlalamikaji kuwa ni kukataa kutii amri ya uhamisho, Mahakama inona kwamba waajiri waliridhika na uzito wa hatua iliyochukuliwa kuhusu suala hilo. Kwa hiyo si jambo la kimsingi kuhusisha uharibifu wa magari na hatua ya kumwachisha kazi mlalamikaji.

Katika hatua nyingie ya madai yao menejimenti wametoa ushahidi kwamba mlalamikaji alikuwa ni mtoro. Kwa mfano terahe 9 Februari, 1979 aliandikiwa barua (Mwajiri Na. 25) ajieleze kwa nini hakuwa kazini tarehe 6, 7, na 8 Januari, 1979. Aliandikiwa barua nyingine tarehe 12 Januari, ambayo ni sehemu ya kielelezo kilichotajwa, ajieleze kwa nini hakuwa kazini tarehe 4, 5, 26 na 27 Januari, 1979. Mlalamikaji alijibu kwamba alikuwa likizoni (local-leave). Aliandikiwa barua nyingine Februari 12, 1979 (Mwajiri Na. 26) ambapo Naibu Meneja Mkuu alionya kwamba mlalamikaji angechukuliwa hatua kwa kudanganya kwamba mlalamikaji angechukuliwa hatua kwa kudanganya kwamba alikuwa kazini siku zilizotajwa kama asingeacha tabia hiyo mara moja. Kwa kuwa hakupeva onyo baada ya mawasiliano hayo ni maoni ya Mahakama kwamba mlalamikaji alijirekebisha.

JUWATA nao wanaendelea kudai kwamba waajiri waliuchukua hatua za haraka na za hamaki kwa kumwachisha kazi kabla ya kupata uthibitisho ambao waliutaka kutoka kwa daktari bingwa. Waajiri waliandika barua ya kutaka ushauri huo kulingana na barua yao Kumb. Na. PF/1573/163/79 ya tarehe 12 Februari, 1979. Katika barua hiyo waajiri walimtaka Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Muhimbili, kutokana na madhara ya mwili aliyokuwa ameyapata mlalamikaji, kumpima kama bado alikuwa ana uwezo wa kufanya kazi. Hii ilikuwa ni siku tano kabla ya umsiamisha kazi mlalamikaji. Kabla Mkurugenzi

Mkuu hajatoa jibu lake menejimenti iliamua kumsimamisha kazi mlalamikaji, kulingana na kielelezo cha Mwajiri Na. 18. Hata alipoachishwa kazi tarehe 3 Machi, 1979 Mkurugenzi Mkuu alikuwa hajajibu. Tunadhani ni kutokana na matukio haya ndiyo maana JUWATA inadai kwamba uamuzi wa waajiri ulikuwa ni hamaki. JUWATA wanadai kwamba kutokana na hamaki hiyo mwanachama wao alikuwa ametakiwa kujibu barua katika muda mfupi kuliko apewao mtumshi anayechukuliwa hatua ya k. 21 (3) (a) na siku saba chini k. 23 (2) Sheria ya Usalama kazini katika ufumbuzi wa masuala ya nidhamu kabla, au mbele, ya baraza la usuluhishi.

Tarehe 25 Aprili, 1980, yapata mwaka mmoja baada kuwachishwa mlalamikaji kazi menejimenti waliandika barua nyingine, wakati huu aone Profesa Hiza, Director of Clinical & Diagnostic Services, hasa wakitaka kujua mambo matatu.

- (a) Iwapo A. A. Kaaya-Physio-Therapist Officer amefuzu na kusajiliwa kama mganga.
- (b) Iwapo physio-therapist alikuwa na mamlaka ya kuandika barua (Mwajiri Na. 16) na isitolewe na Mkuu wa Idara Trauma/Orthopaedic.
- (c) Iwapo tiba ya kucheza viungo (Physio-Therapy) haipatikani katika Hospitali ya Mkoa wa Iringa.

Juhudi yote hii ilifanywa EX POST FACTO kwa kuachishwa kazi mlalamikaji. Baadaye kidogo tutao-na kama hatua hii itawasaidia au haitawasaidia waajiri katika mgogoro huu.

Katika kuwajibu waajiri Profesa P. R. Hiza aliandika barua Kumb. Na. MMC/CDSD/39/C ya tarehe 29 Aprili, 1980. Wakati barua hii inaandikwa mgogoro huu ulikuwa umekwisha tangazwa, na waajiri walijua hivyo kwani barua ya kuutangaza ilinakiliwa kwao. Basi Profesa Hiza alijibu, kwa yale ambayo ni ya muhimu, kwamba Ndugu Kaaya hakuwa na mamlaka ya kuandika barua kwa shughuli kama hii; na kwamba tiba ya kucheza viungo ilikuwa inapatikana Iringa kwa kuwa hata Nurse angeweza kufanya hivyo. Ushauri huu haukuwapo wakati menejimenti wanamwachisha kazi mlalamikaji, kwa hiyo Mahakama inaona kwamba menejimenti ilichukua hatua bila kuwa na ushahidi kwamba mlalamikaji alikataa uhamisho wakati ambapo ngeweza kupata matibabu hayo Iringa.

Mazingara ya mgogoro huu yanafanana sana na yale yaliyokuwa katika Mgogoro Na. 2 wa 1978, NUTA kwa niaba ya mwanachama wao Christian Marijani Mchome dhidi ya Tanzania Breweries Limited. Ushahidi uliotolewa katika mgogoro huo unaonyesha kwamba kampuni ilitoa uhamisho kwa baadhi ya mameneja wa kanda. Ndugu Mchome alikuwa ahame kutoka kanda ya Arusha kwenda kanda ya Shinyanga. Ndugu Mchome alipinga uhamisho kwa sababu nne, lakini sababu kubwa ilikuwa ni ya matibabu. Meneja Mkuu alimtaka Ndugu Mchome atoe cheti cha daktari kuhusu matibabu hayo. Kwa ajili hiyo Ndugu Mchome alipata cheti cha Dr. Rudolf Schmile aliyekuwa anamtibu, kama ilivyokuwa katika mgogoro huu ila tu badala ya kuwa daktari katika mgogoro huu aliyehusika ni mtaalam wa kucheza viungo. Cheti alichopewa Ndugu Mchome kilisema kwamba alikuwa akitibiwa kichocho katika hospitali ya Machame Kwa kujihadhari na uwezokano wa ugonjwa huo kuwa hatari zaidi Ndugu Mchome alishauriwa akae karibu na hospitali hiyo kwa kuwa alikuwa akipata matibabu maalum.

Kwa vile viongozi wa Kampuni waliona umuhimu wa Mchome kwenda Shinyanga haraka, kama ilivyo katika mgogoro huu, Meneja Mkuu alimwandikia Dr. Schemidt tarehe 9 Septemba, 1976 kumuomba afanue kama Mchome alikuwa bado na afya ya kutosha kumwezesha kufanya kazi. Maombi kama hayo katika mgogoro huu alipeleka Profesa Hiza. Pili Meneja Mkuu wa Tanzania Breweries Ltd. (TBL) alitaka kujua kama Mchome angeweza kupata matibabu yale yale huko Shinyanga.

Dr. Schemidt hakujibu barua hiyo, jinsi ambavyo waajiri wa mlalamikaji hapa ambavyo hawakujibiwa barua yao ya mwezi Februari, 1979.

Meneja Maslahi alipokwenda Mchome alipata barua kutoka wa Dr. Moshi, ambaye alikuwa hamtibu Ndugu Mchome ambaye alisema kwamba Ndugu Mchome ange-weza kufanya kazi mahali popote nchini na kupata matibabu katika hospitali yoyote. Barua aliyoandika Dr. Moshi, kama ile ya Profesa Hiza, ilikuwa ni baada ya ya umwachisha kazi mlalamikaji.

Kampuni ya TBL ilidai, kama ilivyodaiwa na ZTRS, kwamba mlalamikaji alikataa kumkabidhi ofisi yule aliyekuwa anakuja kumbadili n.k.

Baada ya kuchunguza nyaraka zote pamoja na ushahidi uliotolewa katika mgogoro huo, Mahakama hii iliamua kwamba hatua ya TBL ilikuwa ni hamaki na ingeweza kueleweka kwamba uongozi wa kampuni ulikuwa unatafuta sababu zozote za kumwachisha Mchome kazi, ingawa uongozi haukuwa na nia hiyo. Mahakama hii inaafiki uamuzi huo na kwamba unahusiana kweli kweli na matukio ya mgogoro huu. Uamuzi katika mgogoro huu ni wa hamaki kubwa. Si wa kimsingi kwa sababu Menejimenti isingekuwa na sababu ya kuendelea kumwachisha kazi iwapo Profesa Hiza angekubaliana na mapendekezo ya Ndugu A. A. Kaaya. Pia Menejimenti haikuwa na jambo lolote mbele yake linalodhihirisha kwamba mlalamikaji angeendelea kupinga uhamisho mbele ya maoni ya Profesa Hiza. Ndiyo maana nase-ma uamuzi ni wa hamaki na s wa kimsingi Kutokana na maoni haya Mahakama inaona kwamba utaratibu uliotumiwa na menejimenti haufai. Utaratibu huo haufai kwa sababu umejidhihirisha kwamba ni wa kimabavu ambao ni mfuko wa uendeshaji usiokuwa na nafasi katika masuala ya usimamiaji wa haki hapo nchini. Kwa ajili hiyo nashindwa kukubaliana hata na maoni ya mshauri wa upande wa waajiri, Ndugu Barkat kwamba menej-menti walimtendea haki mlalamikaji kwa kuchukua hatua hiyo. Tukikumbuka kwamba utawala wa kampuni ya ZTRS ulikuwa ukimpongeza mara kwa mara mlalami-mikaji, na kwamba "you are the only potential person" kuhamia Iringa, si kiendo cha haki kukataa kufikiria na kuzingatia matatizo ya kiafya ya mtumishi wao.

Ni kweli, kama walivyodai waajiri, kwamba mlalami-kaji aliyapata majeraha haya ak'wa nyumbani kwake. Lakini kwa kuwa haupo ushahidi wa kuonyesha kwamba alijitakia kuumia, aliomba na kupewa fidia ya bima inayolipiwa na kampuni. Kama majeraha haya yange-kuwa ni ya kujitakia, na menejimenti ikajua hivyo, uli-kuwa ni wajibu wao kuiarifu Kampuni ya Bima kwamba maumivu au majeraha hayo ni ya kujitakia ili asilipwe fidia. Haki (equity) inadai kwamba mtu yeyote asiru-husiwe kufaidika kutokana na makosa yake. Maadam Menejimenti inaonekana ilijiridhisha kwamba mlalami-kaji hakujitakia kuumia, basi waliuwa na wajibu wa kuona kwamba anatibiwa.

Kutokana na sababu hizi, na jinsi ilivyohukumiwa ka-tika mgogoro wa Mchome, nakubaliana na maoni ya mshauri wa upande wa wafanyakazi kwamba wajiri uli-chukua hatua kali na ya hamaki kubwa mno dhidi ya mlalamikaji. Pamoja na hayo imedhihirika kwamba tabia ya kiburi na matukio kadhaa ya utovu wa nidhamu kwa upande wa mlalamikaji yaliongezea nguvu hatua ya kumwachisha kazi. Isipokuwa ipo tofauti kati ya mgo-goro huu na ule wa Mchome. Katika mgogoro wa Mchome menejimenti ilikuwa imempa uhamisho wa muda walipo-kuwa wakisubiri majibu ya daktari lakini kutokana na tabia yake ya kiburi alikataa kuhama. Ndiyo maana alishushwa cheo aliporudishwa kazini.

Kutokana na sababu zote hizo tunatoa tuzo ifuatayo:

TUZO

Maadamu uamuzi wa waajiri wa kumwachisha kazi mlalamikaji ni batili kisheria; na tukizingatia kwamba, hata mbele ya makosa madogo madogo ya kinidhamu anayohusika nayo mlalamikaji, Mahakama imeridhika kwamba mlalamikaji hakutendewa haki alipoachishwa kazi. Hivyo Mahakama inaibatilisha amri ya kumwachisha kazi mlalamikaji kama ilivyo katika barua ya menejimenti ya tarehe 3 Machi, 1979, Kumb. Na. PF/1573/180/79/rm. Mahakama inaamuru kwamba Ndugu J. K. Pallangyo, mlalamikaji arudishwe (RE-INSTATEMENT) kazini kwa ngazi ya mishahara aliokuwa nao kuanzia tarehe 3 Machi, 1979. Kwa kuwa hana kosa ambalo lingehalalisha hatua ya waajiri, alipwe mishahara yake yote kwa miezi ya nyuma, yaani kuanzia Machi, 3, 1979 hadi leo na kuendelea kila mwezi atakaokuwa mtumishi.

Iwapo waajiri bado wanataka ahame, basi mlalamikaji ahame mara moja bila kuchelewa.

Imetolewa leo hii tarehe 19 Novemba, 1980 na inakuwa na nguvu za sheria mara moja.

Dar es Salaam,
19 Novemba, 1980

J. J. M. MACKANJA,
Naibu Mwenyekiti,
Mahakama ya kazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 524

HATI ZA UVUMBUZI

Sheria ya (Uandikishaji) Uvumbuzi Usiigwe
(Sura ya 217)

Inatangazwa kwa watu wote kwamba hati za uvumbuzi zenye maelezo yaliyomo kwenye Nyongeza ya Tangazo hili zililandikishwa kuwa Nambari 2093 ya 1981 katika Daftari la Tanganyika la kuandikisha hati za uvumbuzi mnamo tarehe 9 mwezi wa Mei, 1981.

NYONGEZA

Nambari ya ombi: 3093.

Tarehe: 4 Mei, 1981.

Jina la muombaji: HOECHST AKTIENGESELLSCHAFT.

Anwani iliyoandikishwa: 6230 Frankfurt/Main 80, Postfach 80 03 20, Federal Republic of Germany.

Maelezo ya kukubaliwa katika Ulaya ya Uingereza:

Hati ya uvumbuzi Na. 1565894 iliyotwa muhuri tarehe 25 Juni, 1980 Uingereza.

Aina ya kitu kilichovumbuliwa: Pesticidal organic phosphorus compounds, processes for their preparation and compositions containing them.

Hati, n.k. zilizowasilishwa kwenye masjala:—

1. Hati ya maa nisho ya uvumbuzi iliyohakikishwa kutoka Uingereza.
2. Hati ya Msimamizi Mkuu wa Ofisi ya Uvumbuzi kutoka Uingereza.
3. Idhini ya wawakilishi: Donaldson & Wood, S.L.P. 176, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
9 Mei, 1981

T. K. MAKATA,
Msajili Msaidizi wa Uvumbuzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 525

KAMPUNI ZINAZOTARAJIWA KUFUTWA KATIKA DAFTARI LA MAKAMPUNI

Sheria ya Makampuni

(Sura ya 212)

Inatoewa ilani chini ya kifungu 283 (3) cha Sheria ya Makampuni, kwamba kampuni zifuatazo zitafutwa katika Daftari la Makampuni iwapo hakutatokea kipingamizi chochote baada ya miezi mitatu kupita tokea tarehe ya ilani hii.

GHOHAN INVESTMENTS LTD.
UNITED QUARRIES LTD,
TANGANYIKA TEGRY PLASTICS LTD.
THE TANGA BOHRA INVESTMENT SOCIETY LAD.
DAIRIES LIMITED.
ANPURNA LIMITED.
KASSAMALI ISMAIL & AGENCIES (T) LTD.
J. P. PATEL & COMPANY 1962 LTD.
AMBASSADEUR CINEMA (IN LIQUIDATION).
PROPERTIES & INVESTMENT LTD.

Dar es Salaam,
15 Mei, 1981

T. K. MAKATA,
Msajili Msaidizi wa Makampuni

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 526

ALAMA ZA BIASHARA ZILIZOANDIKISHWA KATIKA DAFTARI

Alama za biashara zilizotajwa hapo chini zimeandikishwa katika daftari la alama za biashara mwezi Aprili, 1981.

Nambari	Daraja	Mwenye Mali
18374	5	Roche Products Limited.
17720	3	Faberge Incorporated.
18379	6	T.H. Holoschmidt A.G.
18383	16	Wiggins Teape Limited.
18173	3	Unilever Limited.
18344	5	E. R. Squibb & Sons Inc.
18353	5	May & Baker Ltd.
18163	5	Unilever Limited.
18065	33	John Burkmaster & Sons Limited.
18376	5	May & Baker Limited.
17482	5	C. H. Boehringher Sohn.
17702	9	Varian Associates Inc.
17860	29	Hubbard Europa B. V.
15128	5	Bas Aktiengesellschaft.
12310	23	Adamjee Industries Limited.
16799	5	Celamerck GMBH & Co. KG.
18320	5	Reckitt & Colman (Over Seas) Limited.
18367	34	Balenciaga, Societe Anonyme.
17702	9	Varian Associates Inc.
B17349	5	Janoowalla Chemists Ltd.
17499	5	Nuruddin M. Janoolwala and Aziz M. Janoowalla.
18321	3	Beckitt & Colman (Over Seas) Limited.
16800	5	Celamerck GmbH & Co. KG. A. Kommanditgesellschaft.
18354	5	Roche Products Limited.
17502	5	Nuruddin M. Janoowalla and Azizi M. Janoowalla.
18186	5	Southells (Birmingham) Limited.
14669	1	Ciba-Geigy Limited.
15853	33	Ettablissement Marqint Grandes Marques Internationals.
17722	32	Anheuser-Busch Incorporation.
B.18057	5	Beiersdori Aktiengesellschaft.
18441	5	Golgate-Palmolive Company.
17874	5	Roche Products Limited.
16361	12	Rolls-Royce Limited.
18333	1	Hoechst Aktiengesellschaft.
18387	5	Johnson & Johnson.
17722	32	Anheuser-Busch Incorporated.
18369	20	Afro Crafts and Curios.
12310	23	Adamjee Industries Limited.
17582	6	Boc Limited.

Dar es Salaam,
Mei, 1981.

T. K. MAKATA,
Msajili Msaidizi wa Alama za Biashara.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 527

ALAMA ZA BIASHARA ZILIZOANDIKISHWA KATIKA DAFTARI

Alama za Biashara zilizotajwa hapa chini zimeandikishwa upya katika Daftari la Alama za Biashara Mwezi Aprili, 1981.

Nambari	Daraja	Mwenye Mali
1238	40	The Good year Tire and Rubber Company
17149	20	Vita International Limited.
17129	30	Guigoz S.A.
17020	5	S.C. Johnson and Son Inc.
1 74	5	Co-oper Mc Dougall and Robertson Limited.
15480	30	CPC International Inc.
17122	1	Imperial Chemical Industries Limited.
15315	16	Caribonum Limited.
15408	1	Chubb fire security Limited also trading as Read and Campbell.
3593	43	Martini and Rossi S.P.A.
3554	5	Winthrop Products Inc.
3592	43	Martini and Rossi S.P.A.
6699	16	Imperial Chemical Industries Limited.
6698	10	Imperial Chemical Industries Limited.
6700	22	Imperial Chemical Industries Limited.
6174	5	The boots Company Limited.
5972	5	The boots Company.
6617	5	C.H. Boehringer Sohn A A Kommanditgesellschaft.
6593	33	Martini and Rossi S.P.A.
235	20	Imperial Chemical Industries Limited.
14323	5	Eli Lilly and Company.
6090	20	Formica International Limited.
6089	19	Formica International Limited.
3594	43	Martini and Rossi S.P.A.
6607	30	Fleer Corporation.
3717	43	Taylor and Ferguson Limited.
5652	7	The Singer Company.
5660	20	The Singer Company.
5654	20	The Singer Company.
5663	7	The Singer Company.
12812	30	Hall Brothers (Whitefield) Limited.
12811	5	Hall Brothers (Whitefield) Limited.
6533	34	J. R. Freeman and Son Limited.
6530	34	J. R. Freeman and Son Limited.
5996	3	Henkel Kommanditgesellschaft AUF Aktien.
3245	6	Imco Osterreichische Feuerzeug-ung Metta watenfabrik J. Meister and Co'll-
3708	3	John Wyeth and Brother Limited.
15275	5	Basf Aktiengesellschaft.
1233	13	BOC Limited.
3268	40	Messrs Mitchell Cotts Kenya Limited.
3567	47	Messrs Colgate-Palmolive Company.
3699	48	Messrs Colgate-Palmolive Company.
248	6	Dunlop Limited.
250	40	Dunlop Limited.
249	13	Dunlop Limited.
251	49	Dunlop Limited.
17190	34	Agio Sigarenfabrieken N.V.
17135	5	E. R. Squibb and Sons Inc.
3714	40	Dunlop Limited.
3718	20	Imperial Chemical Industries Limited.
B14430	34	Robinson Hotels GmbH.
B14425	16	Robinson Hotels GmbH.
6719	3	Goya Limited.
17125	5	Beecham Group Limited. Trading also as Beecham Agricultural Products.
6475	33	Messrs George Ballantine and son Limited.
6799	1	Imperial Chemical Industries Limited.

Dar es Salaam,
14 Mei, 1981

T. K. MAKATA,
Msajili Msaidizi wa Alama za Biashara

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 528

MAOMBI YA LESENI ZA MAGARI YA ABIRIA, UCHUKUZI WA MIZIGO NA MABADILIKO YA LESENI

Kutokana na kifungu cha Sheria za Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973 (The Transport Licensing Authority Act, 1973) ninakujulisha kwamba utaratibu kama ulivyo-pangwa katika orodha ya leseni kama ifuatavyo:—

Mtu yeyote anayehusika na kifungu cha Sheria za Leseni za Usafirishaji na ambaye angependa kupinga maombi haya apeleke maombi yake ya kupinga katika Ofisi ya Katibu, Mamlaka ya Utoaji Leseni za Usafirishaji, S.L.P. 674, Mbeya. Maombi ya namna hiyo yamfikie Katibu kabla ya siku kum na nne tokea tarehe ya kutangazwa kwa taarifa hii. Maombi ya namna hiyo yawe kama vile ilivyoonyeshwa katika fungu la 33 (2) la Sheria za Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973. Nakala za fomu zinapatikana katika Ofisi ya Mamlaka za Usafirishaji.

ORODHA

(Angalia: R.S.L. = Leseni za Magari ya Abiria.

P.C.L. = Leseni za Uchukuzi wa Mizigo),

MB/01662—Mwakwenda Mwangonela, S.L.P. 892, Mbeya. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mkoani Mbeya.

01663—Roger Mwansile, S.L.P. 147, Mbeya. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mkoani Mbeya.

01664—Julius A. Mbarama, S.L.P. 4, Rujewa. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la $\frac{3}{4}$ tani katika barabara za Mkoani Mbeya.

01665—Andiel Shonza, S.L.P. 66, Mbozi. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 1 katika barabara za Mkoani Mbeya.

01666—Samson W. M. Shonyela, 816, Mbeya. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 26 safari za mara kwa mara kutwa kutoka Mbeya Mjini mpaka Mwakibete kupitia Mwanjelwa.

01667—Bernad Staub, S.L. Pekee, Mbozi. Ombi la kuendeleza leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 7 katika barabara za Mkoani Mbeya (A/MB/0348/79).

01668—Alleni J. Mwakyoma, S.L.P. 505, Mbeya. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mkoani Mbeya.

01669—Ndawayo Sanga, S.L.P. 419, Mbeya. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 1 katika barabara za Mkoani Mbeya.

01670—Ndawayo Sanga, S.L.P. 419, Mbeya. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mkoani Mbeya. (B/MB/0462/79).

01671—Emmanuel Mwansasu, S.L.P. 74, Tukuyu. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani $1\frac{1}{2}$ katika barabara za Mkoani Mbeya.

01672—E. S. J. Mkumba, S.L.P. 1083, Mbeya. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani $1\frac{1}{2}$ katika barabara za Mkoani Mbeya.

01673—Sadrudin K. Jessani, S.L.P. 15, Tukuyu. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 5 katika barabara za Mkoani Mbeya.

Y. E. MKOMA,
k.n.y. Katibu,

Mamlaka ya Leseni za Usafirishaji. Mkoani Mbeya

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 529

MAOMBI YA LESENI ZA MAGARI YA ABIRIA. UCHUKUZI WA MIZIGO NA MABADILIKO YA LESENI

Maombi ya leseni za Magari ya Abiria, Uchukuzi wa mizigo na mabadiliko ya leseni katika Mkoa wa Dodoma.

Mtu yeyote anayehusika na kifungu cha Sheria za Usafirishaji na ambaye angependa kupinga katika maombi haya apeleke maombi ya kupinga katika Baraza la Mkoa la Utoaji Leseni za Usafirishaji, S.L.P. 953, Dodoma. Maombi haya yafike katika Baraza hili (Regional Transport Licensing Authority) kabla ya tarehe 30 Januari, 1981.

ORODHA

(Angalia: R.S.L. = Leseni za Magari ya Abiria.

P.C.L. = Leseni za Magari ya Uchukuzi wa Mizigo).

DO/0942—Laabed M. Tamim, S.L.P. 87, Dodoma. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0943—Abdallah Hassani, S.L.P. 509, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo wa gari 1 la tani 5 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0945—Bakari Omari, S.L.P. 1090, Dodoma. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0946—Juma Mohamed, S.L.P. 52, Kondoa. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1½ katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0947—Omari Salum, S.L.P. 375, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 5 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0948—Jaffer H. L. Ladak, S.L.P. 41, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 2 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0949—Hamisi Mfaume Risasi, S.L.P. 274, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 3 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0950—Salehe Mohamed Bagoza, S.L.P. 57, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0951—Moris Alois Kisoli, S.L.P. 1574, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0952—Said Salum, S.L.P. 49, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0953—Abdallah Hassan Sangali, S.L.P. 93, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 3 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0954—Omari Abdallah & Juma Ali, S.L.P. 128, Kondoa. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 7 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0955—Joseph Boshe, S.L.P. 482, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0956—Akian F. Abdallah, S.L.P. 411, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa magari 2 ya tani 7 kila moja katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0957—Ibrahim Abwana, S.L.P. 99, Mpwapwa. Ombi la leseni ya abiria kwa Bus 1 la abiria 60 katika njia za kutoka (i) Kinusi mpaka Mpwapwa kupitia Chogola, Kibakwe na Gulwe (ii) Pingarame mpaka Kinusi kupitia Kongwa, Mpwapwa na Kinusi.

DO/0958—Daniel John Liacho, S.L.P. 529, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 5 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0959—Salum Mohamed, S.L.P. 87, Dodoma. Ombi la leseni ya abiria kwa Bus 1 la abiria 60 katika njia za kutoka Ikasi mpaka Dodoma kupitia Igangu, Chali na Chipanga.

0960—Hassan Omar Mapesa, S.L.P. 1328, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 3 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0961—Willy Mwanga na A. Malya, S.L.P. 835, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0962—Kampuni ya Usafirishaji na Uchukuzi, S.L.P. 271, Dodoma. Ombi la kuendeleza leseni ya abiria kwa Mabasi 8, 3 ya abiria 65, 5 ya abiria 60 katika njia za (i) Dodoma, Kondoa, Kwadelo na kurudi Dodoma; (ii) Dodoma, Mpwapwa, Mlali na kurudi Dodoma, (iii) Dodoma, Kibore na kurudi Dodoma; (iv) Dodoma, Kondoa, Itaswi na kurudi Dodoma; (v) Huduma za Town Bus Mjini Dodoma.

0963—Nicolaus Ulawe, S.L.P. 1005, Dodoma. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa magari 2, moja la tani 7 na tani 5 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0964—Abdulkadri Haji Abdillali, S.L.P. 126, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 1½ katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0965—Alexander Kanyamala, S.L.P. 130, Dodoma. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa magari 3 ya tani 7 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

0966—Issa Miat, S.L.P. 19, Kongwa. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari 1 la tani 3 katika barabara za Mkoa wa Dodoma.

Z. S. MTENGETI,

Mjumbe,

Dodoma,
28 Aprili, 1981

Baraza la Leseni za Usafirishaji
Dodoma

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 530

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Dar es Salaam)

SHAURI NA. 16 LA MWAKA 1981

Maombi ya barua za usimamiaji wa mirathi ya Kantilal Dwarkadas Pandya, marehemu

Lataben Kantilal Pandya na Rajendra Kantilal Pandya, Waombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

